


WAKATI WA KANISA LA SARDI

 . . .mfalme. Ndugu yangu alikuwa tu akiniambia ya kwamba kulikuwako na hizi lesu, kwa ajili ya mtu fulani anayekufa kwa kansa. Kwa hiyo tutakuwa tukiwaombea katika muda mfupi tu. [Ndugu Neville anasema, “Kuna haja mbili papo hapo upande huo mwingine.”—Mh.] Haja mbili? Vema, nitaninii. . . [“Moja ya hayo. Hiyo moja ni haja.”] Vema, bwana. Nami nitaziweka hapo kuziombea pia.

² Ndipo basi ndio kwanza mtu fulani apitishie muhtasari, amekuja huku na kupitisha muhtasari juu ya hilo. . . kuhusu ibada kesho. Ninyi mlio hapa mnaotutembelea, hakika tungependa mshuke mje alasiri saa nane, kesho alasiri, watakuwa na ibada za kanda. Na endapo hufanyi lolote, kutakuwako na mmoja wa jumbe hizi ambao—ambao hujawahi kusikia utakaochezwa na kufanya mkutano wa mombi, na—nasi tutatarajia tu wakati mzuri kesho alasiri saa nane. Utakuwa ni wakati wenye shughuli nyingi kwangu maana kesho, mnaona, sina budi kuchukua Jumapili asubuhi, na pia Jumapili usiku, na kesho usiku, pia, na historia yote juu ya makanisa hayo.

³ Na sasa, Jumapili asubuhi, Bwana akipenda, tunatarajia wakati mzuri sana, maana Jumapili asubuhi ikiwa ni pumziko letu, namna ya pumziko kutoka Jumamosi usiku. . . ni Wakati wa Kanisa la Laodikia. Lakini Jumapili asubuhi ninataka kuchukua: *Mwanamwali Aliyelala*, na *Ufufuo*, *Wale wanne*. . . *Mia na Arobaini na Nne Eflu*, na maskini sehemu hizo zote legevu zinazoufunganisha ujumbe pamoja kwa ajili ya Jumapili asubuhi. Ibadu zitaanza saa tatu. Hiyo ni kweli, mchungaji? Saa tatu, Jumapili asubuhi, ambapo tunataka kuyachukua mambo hayo yote kama “Itakuwaje kwa huyo mwanamwali aliyelala, na itakuwaje kwa mwanamwali mwenye busara? Watarudi lini? Ama wale mia na arobaini na nne elfu wataonekana wapi?” Na mambo mengi kama hayo kwa ajili ya Jumapili asubuhi, kujaribu kufunganisha hayo pamoja, ambayo hayo yanaambatana moja kwa moja na ujumbe huu. Na ndipo Jumapili usiku tutamchukua yule malaika mkuu wa mwisho na Ujumbe kwa Laodikia, Jumapili usiku, Bwana akipenda.

⁴ Na sasa, basi, kesho alasiri ni ibada hapa, ibada ya kanda. Ndugu Gene ndio kwanza aniambie ya kwamba wangeninii. . . tutaanza saa nane kesho alasiri. Nanyi watu mnaotaka kuja hapa kusikiliza hizo jumbe, mwe na maombi madhabahuni, ninyi ambao mnamtafuta Roho Mtakatifu ama kitu fulani, wakati wa ajabu sana. Kanisa ni zuri na joto, limefunguliwa, na tayari kwa mtu yeyote wakati wowote anayetaka kuingia na kuomba na kumtafuta Bwana. Kanisa li wazi na linangojea.

Nasi tunaninii. . . tutakuwa tukiwatarajia, tuliweke jinsi hiyo, tutakuwa tukiwatarajia kesho alasiri.

⁵ Ama wakati wowote mnaotaka kuja kanisani kuomba, mbona, daima liko tayari. Na ikitokea kwamba milango imefungwa ama kitu fulani, upande wa pili wa barabara hapa tu, ndugu yangu, ambaye ndiye mwangalizi hapa. Nafikiri ni 411, ninaamini hivyo. . . Ama 811 (hiyo ni ninii. . .?) 811, yapata tu hatua chache kutoka hapa kanisani, 811. Mbona yeye, ninii. . . mke wake angekuwa na ufunguo kama wakiuvuta mlango pamoja nao ujifunge, bali wao huuacha wazi labda asubuhi, wanaufungua. Ama, baada ya ibada, unafungwa usiku, kuwazuia watoto wasikimbie ndani, mwajua, na kuvunja madirisha na kadhalika; mnajua jinsi watoto walivyo, hasa sana katika siku hizi. Kwa hiyo sisi huufunga kwa sababu hiyo. Tunachukia kulazimika kufunga mlango wa kanisa wakati wowote. Labda wakati lile lingine litakapomalizika, tutalifanya ili labda lipate kuwa tofauti basi, na sisi. . . mtu fulani anaweza kuwa pale wakati wote kusudi watu waweze kuja na kuomba, na kutafuta uponyaji, kumtafuta Roho Mtakatifu.

⁶ Ninyi, msio na Roho Mtakatifu maishani mwenu, shukeni mje, mkae hapa, kaeni tu usiku kucha mkitaka, kaeni tu mpaka mtakapompokea.

⁷ Ni nani yule aliyekuwa hapa muda mfupi uliopita akiimba, “Mungu juu ya nafsi yangu yote, na Mungu kila mahali”? Ni—nilifikiri Unyakuo ulikuwa umekuja; mimi, nikaangalia kote kule, nione kama kila mtu alikuweko. Ulikuwa ni mzuri sana; ninauthamini huo. Tungestahimili huo kidogo karibu tu wakati wote. Naam, bwana. Hiyo ni. . . Ndiyo kwanza niingie, wakati wa kuanza kuusikia huo.

⁸ Nami nimekosa kuimba kote kuzuri katika mikutano hii kwa sababu nilifikiri ya kwamba labda. . . Loo, nina shughuli nyingi sana, mnajua jinsi ilivyo. Watu—watu wanakuja kwa ndege, kwa garimoshi, kwa. . . Nyinyi—nyinyi hamjui hilo, mnaona, maana inakuja tu kwa simu, inakubidi kuwaendea, ukutane nao na kuwaombea, na kila mahali. Inaendelea tu sikuzote, halafu kujaribu kusoma pia; inakuwa ni shida sana. Lakini daima tuna furaha kukutana na watu na kufanya tuwezalo kwa ajili yao kwa sababu ni. . . hiyo ni ninii yetu. . . sisi ni watumishi wa umma kwa ajili ya Bwana Yesu Kristo kwa watu Wake katika siku hii. Nasi tunapenda kufanya zaidi ya yale kweli tufanyayo, bali hatuwezi.

⁹ Mhudumu alikuja upesi asubuhi ya leo, amechanganyikiwa kabisa, ameharibikiwa kabisa, jamaa mzuri. Na kwa sababu kwamba alikuwa. . . alifanya tu kazi kupita kiasi. Akapata. . . Akaanza kuamka, naye msichana wake mdogo alikuwa amesimama chumbani, msichana akaanza kuzunguka-zunguka kasi. Alikuwa amevaa pajama ndogo nyekundu; anasema

jambo la mwisho analokumbuka lilikuwa ni doa dogo jekundu likizunguka, na kuzunguka, na kuzunguka, na kuzunguka, namna hiyo. Akazimia, mnaona. Kwa hiyo wakamleta huku mbio. Kwa hiyo ni—ni kazi nyingi kupita kiasi, mnaona. Ku—kumbuka wewe ni mwanadamu na sisi—sisi tunataka... tunafikiri mzigo wote umewekwa juu yetu. Lakini, mwajua, Mungu anao watumishi kila mahali kushughulikia baadhi ya hayo, na kwa hiyo tunafanya tu vizuri tuwezavyo. Lakini mhudumu mzuri akijaribu kufanya yote awezayo katika siku hizi za mwisho kwa ajili ya Bwana wake. Hakika mimi... Naye Bwana akamkomboa papo hapo, yeye ni mzima tu, akamrejsha kabisa, mzima, mwenye afya, akaenda zake, akishangilia.

¹⁰ Na, loo, jambo kubwa lilitukia leo. Sitaki tu kuanza mambo hayo, lakini... Mwajua, nilimwambia mke wangu, nikasema, “Sasa, kutakuwa na mtu atakayekuja pale, naye atakuwa ni mwanamume, mfupi, mnene, nywele nyeusi na macho meusi, atasoma ubao ule na aanze kuninii... bali wewe mwite, unaona.” Nikasema, “Kwa sababu Bwana ana ujumbe kwa ajili yake.” Nami nikainua Biblia na kuifungua, na nikasema, “Nitayaweka mambo haya hapa ndani kusudi uone hivyo ndivyo hasa Bwana anataka yeye afanye.”

¹¹ Miaka minane iliyopita, Mpoli kutoka Polandi, alilelewa Polandi... Mkutanoni, alikuja jukwaani nao wakasema... ama Roho Mtakatifu alimwangukia, akamwambia, akasema, “Umechanganyikiwa tu.” Hiyo ni... Yeye alifikiri nililisema, bali ni Roho Mtakatifu aliyesema. Lilikaa ndani yake tangu hapo, na hatimaye likamvuta kutoka Jiji la Kansas hadi humu jengoni jana usiku, na ndipo akachanganyikiwa kabisa hapo aliposikia juu ya ubatizo huo wa maji. Akaenda kwenye hoteli yake, ndipo Roho Mtakatifu akasema, “Simama sasa uende pale juu.” Mtu fulani alitaka kuja pamoja naye, bali akakataa kwa sababu katika ono alikuja peke yake. Mnaona? Na kwa hiyo... naye, kama muungwana kusoma ubao, alianza, akageuka aende, naye mke wangu akamwita nami nikaenda mlangoni, nikasema, “Huyo—huyo ndiye, acha aje.”

¹² Akasema, “Nifanye nini?” Akiisha kuona, akasema, “Sasa ninauona.”

Nikasema, “Ninataka kukuonyesha hili upate kujua sasa, unaona.” Nikasema, “Bwana aliniambia ulikuwa unakuja.” Mnaweza kumwuliza. Nikasema, “Sasa, haya hapa Maandiko. Yasome papa hapa kabla hujaendelea.”

¹³ Vema, yupo hapa kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo sasa. Kwa hiyo...?... Huenda ameketi hapa sasa, nijavyo mimi. Uko hapa, ndugu? Ndugu, ndugu Mpoli. Huh? Naam, huku nyuma pembeni huyu hapa, naam. Simama... inua mkono wako ili waweze kukuona hapo. Vema. Kumwona Roho Mtakatifu... Hayo hutukia tu wakati wote. Watu wengi hufikiri ya kwamba

maono huja tu jukwaani. Loo, hilo halilianzishi. Vipi kuhusu hilo, Ndugu Leo? Kila mahali tu, mnaona. Vema, hapa ni mahali padogo Pake, hapa. Hapa ni mahali ambapo kidogo sana hufanyika. Huko nje ndiko linaendelea mchana kutwa na usiku, mnaona. Naam, mwulizeni mke wangu, naye... ama hao, na jirani yangu pale nyuma, Ndugu Wood, na hao wote walioko huku. Loo, jamani! Haya ni mambo ma—madogo hapa; mambo makubwa ndiyo yanayotukia huko. Sasa, wala nusu haijapata kusimuliwa bado. Loo! Nina furaha sana kwa ajili yake, nikijua ya kwamba Bwana wetu hivi karibuni anakuja nasi tutakuwa pamoja Naye daima basi; sio *daima*, bali *Milele*, Milele.

¹⁴ Sasa, Bwana akipenda, ninaamini ni tarehe kumi na nane, Jumapili, juma moja. Jumapili, juma moja, tarehe kumi na nane. Nimekuwa na vita vibaya sana; Shetani amejaribu kunipa homa hii ambayo inaenea huku, ninakazana tu kumrudishia; naye ananikabidhi, nami ninamrudishia. Kwa hiyo... na kwa hiyo nimekuwa na vita kwelikweli. Kwa hiyo labda tutapambana juma lijalo. Halafu basi, Bwana akipenda, ifikapo Jumapili ijayo, tarehe kumi na nane. Nasi tutajaribu kuleta ibada ya kuwaombea wagonjwa maana wananinii... mambo yanalundikana na kulundikana na yale ya dharura kabisa tunajaribu kuyashughulikia upesi tuwezavyo, na majira, majira yote ya usiku na kila kitu kinachokuja na kuondoka. Kwa hiyo tarehe kumi na nane tutafanya ibada ya kawaida ya uponyaji. Na endapo una baadhi ya wapendwa wako wanaotaka kuombewa, vema, walete huku, ama uwalete wakati huo.

¹⁵ Sasa, kuna jamaa wengi wa Jeffersonville waliokuwa wakiniambia, wakasema walikuja wakati mzuri wa kufika hapa, yapata saa kumi na moja, wakasema hakuna hata nafasi kuyaegeshea magari yao (ama thenashara). Kwa hiyo wao... Nikasema, “Vema, ninyi... Hawa ni ndugu wageni wetu kutoka kila mahali, watu, wahudumu wengi.” Nikasema, “Wana—wanashikilia mafundisho ya Hili.”

¹⁶ Nasi tunajaribu tu kugusia mambo yaliyo muhimu. Halafu baadaye kidogo, mbona, tutayaweka kwenye kitabu mpate kuyasoma na—na kitakuwa na mengine zaidi ki—kidogo yataongezewa, kwa sababu usiku... Mnaona, siku kadhaa usiku zilizopita, nimekuwa nikijaribu, nimekuwa, kuiokoa sauti, mnaona, kwa sababu upeo huo mkubwa, huo ndio ninaotaka kuona; pale ambapo ufunuo wa Kristo utafanywa katika wakati huu, mnaona, kile ulicho.

¹⁷ Na sasa, kabla hatujaanza kuyasoma Maandiko... Nami najua kesho ndiyo ile siku kubwa ya kibiashara ambapo inatubidi sote kwenda kununua vyakula vyetu vya Jumamosi usiku. Nasi hatuna budi kuvinunua Jumamosi alasiri ama Jumamosi asubuhi, mojawapo, ili tuweze kuwa huru Jumamosi usiku kuja kanisani. Kwa hiyo tutajaribu kuwaachilia mapema usiku wa leo kusudi msiwe mmechoka sana kesho kuvipata,

kisha mrudi kwenye ibada ya alasiri pamoja na ndugu hapa walio na kanda na—na pia kwa ajili ya kesho usiku.

Sasa, tunaweza tu kusimama dakika moja kwa ajili ya maombi, mkiweza.

¹⁸ Sijui, kabla hatujaomba, kama kuna mtu yeyote hapa aliye na haja maalumu ya maombi, kama tu utafanya ijulikane kwa mkono ulioinuliwa. Mungu anaona. Sasa mnaona kama tuko katika ulimwengu mhitaji ama la, enyi ndugu. Nakisia asilimia tisini na tano ama tisini na nane ya wasikilizaji iliinua mikono yao basi kwa . . . Sasa, kumbukeni, huwezi hata kusogea pasipo Mungu kujua hilo. Mnaona? Yeye alijua nia yako, alijua ulichokuwa ukiombea.

Na tuinamishe vichwa vyetu:

¹⁹ Baba Mwenye Rehema wa Mbinguni, tunaukaribia Utakatifu Wako usiku wa leo, Kiti Chako cha Enzi, kwa ahadi yako ya kwamba ulisema ungesikia. Na kama tungeamini, ungetupa tulichoomba. Nasi tunakiri makosa yetu yote. Tunatambua, Bwana, kwamba ha—hatustahili yoyote ya baraka Zako. Ha—hatustahili. Hatustahili kabisa, wala hatuji kana kwamba tu—tulistahili na—na tumefanya jambo kubwa. Ee Baba, tunapoangalia Kalvari, hiyo inaondoa ukuu wote kutoka kwetu, ha—hatujui kitu kingine basi ila Kristo Naye amesulubiwa. Ndipo tunapona ya kwamba alifufuka siku ya tatu kulingana na Maandiko, kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu, akarudi siku arobaini baadaye katika umbo la Roho Mtakatifu, apate kukaa nasi mpaka kuonekana Kwake dhahiri angani wakati wa mwisho. Nasi tunauona huo wakati wa mwisho ukikaribia upesi sana sasa. Nasi ni watu walio na furaha sana, Bwana, kwa sababu kwamba—kwamba Wewe umetupatia baraka hii kuu.

²⁰ Ninashukuru sana, Baba, ya kwamba kusanyiko hili linalosikiliza limeketi na mioyo iliyoimamishwa, na kusikiliza . . . ? . . . Halafu basi, Bwana, ninaomba ya kwamba utaitakasa midomo yangu usiku wa leo, na kila usiku na kila wakati ambao nitakuja mimbarani Mwako kusema na watu Wako; kwa sababu, Bwana, kamwe usiniache niseme lolote lisilo sahihi. Ungali una nguvu za kuifunga midomo kama ulivyofanya kwa Danieli kwenye tundu la simba. Na kama kamwe nikisema lolote lisilolingana na mapenzi Yako, kifunge kinywa changu, Bwana, nisije nikalinena. Yapite mawazo yangu; niweke kwenye njia ifaayo, Bwana, ambapo sitasema kitu ila Kweli. Kwa kuwa ninatambua ya kwamba katika ile siku kuu watu hawa watakuwa wakingojea huko ng'ambo juu ya ninii . . . wakingojea kulingana na huduma ambayo nimewahubiria. Kama ukija ku—kuchukua moja ya nyota Zako, na malaika Wako, wahudumu Wako, watumishi Wako, itawabidi

kucharazwa kwanza kulingana na Jumbe hizi ambazo tumekuwa tukihubiri hapa. Utawawajibisha, watumishi Wako.

21 Sasa, Baba, ninaomba ya kwamba utamjalia Roho Mtakatifu kunena na si mwanadamu. Itahiri mioyo yetu tupate kumsikia. Nitakuwa nikisikiliza, Baba. Naomba kwamba utawaponya wagonjwa na wanaoteseka. Watu wote walio wahitaji, kila mahali, jalia neema Yako na rehema ziwe pamoja nao. Jalia kila haja iliyofanywa ijulikane usiku wa leo kwa mkono ulioinuliwa. Kote nchini wakati wengi zaidi wanateseka, hata wale ambao lesu hizi zinawakilisha, na maombi haya yaliyowekwa chini ya mkono wangu hapa, jalia Roho Mtakatifu ajibu, Baba, na kuwaponya wagonjwa. Nena nasi sasa kupitia kwa Neno Lako lililoandikwa, kwa Roho Mtakatifu, tunaomba katika Jina la Yesu. Amina. Ketini.

22 Sasa, usiku wa leo kidogo kuna joto kanisani. Ule Wakati mkuu wa Kanisa la Laodikia ukija. Na usiku wa leo tunaukaribia ule wakati mwingine mkuu wa kanisa ambao utakuwa ni—ni wakati wa tano wa kanisa. Tumechukua wakati wa kwanza wa kanisa, ambao ni Efeso. Huenda nikasoma haya tena mwanzoni, yote yaliandikwa na kwa hiyo ningetaka kuwasomea yote hapo ninyi ambao mnetaka kuyachunguza kwenye karatasi zenu.

23 Wakati wa kwanza wa kanisa ulikuwa ni Wakati wa Kanisa la Efeso, kuanzia A.D. 55 hadi 170. Paulo akiwa ndiye nyota, nao ulikuwa ndio wakati wa kwanza wa kanisa. “Matendo pasipo na upendo” yalikuwa ndiyo malalamishi ya Mungu. Zawadi ilikuwa “Mti wa Uzima.”

24 Wakati wa pili wa kanisa ulikuwa mwaka wa 170 hadi 312, Ireneo alikuwa ndiye mjumbe wa siku hiyo. Nayo malalamishi yalikuwa mates- . . . yalikuwa ni dhiki, na kanisa lililoteswa. Zawadi, “Taji ya Uzima.”

25 Wakati wa tatu wa kanisa ulikuwa ni Pergamo, Mtakatifu Martin akiwa ndiye mjumbe wa kanisa hilo. Wakati huo wa kanisa ulikuwa ni kutoka mwaka wa 312 hadi 606. Lalamiko lilikuwa ni “mafundisho ya uongo, uongo wa Shetani, msingi wa utawala wa Kipapa, nayo ndoa ilikuwa ni ya kanisa na nchi pamoja.” Zawadi ilikuwa ni “mana iliyofichwa, na jiwe jeupe.”

26 Nao wakati wa nne wa kanisa ulikuwa ni wa Thiatira; Columba akiwa ndiye malaika wa wakati huo wa kanisa, mjumbe wake; mwaka wa 606 hadi 1520. Nao wakati huo wa kanisa ulikuwa ni ushawishi wa Kipapa, Nyakati za Giza. (Ilikuwa jana usiku, mwajua, Nyakati za Giza.) Nayo za—zawadi, ilikuwa “mamlaka ya kuyatawala mataifa, na Nyota ya Asubuhi,” kwa malaika huyo.

27 Sasa, usiku wa leo, tunaanzia kwenye wakati wa tano wa kanisa, ambao ni wakati wa kanisa la Sardi, S-a-r-d-i, Sardi. Naye mjumbe wa wakati huu wa kanisa alikuwa ni Martin Luther, anakuwa mwenye kufahamika vizuri zaidi kwa msomi

wa Biblia ama mwalimu huyu, ama walei, hasa, siku hizi. Nao wakati huo wa kanisa ulianza katika mwaka wa 1520 na ukaisha 1750, 1520 hadi 1750; na wakati wa kile tunachokiita “Wakati wa Matengenezo.” Nalo lalamiko lilikuwa “Kutumia jina lao wenyewe.” Nayo zawadi ya hao masalio wachache waliosalia, ilikuwa “Kutembea mbele Zake wamevaa vazi jeupe, na majina yao kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo.” Bwana na atubariki tunapoanza sasa.

²⁸ Sasa tutaanza kwenye kifungu cha kwanza cha mlango wa 3, wa wakati huu wa kanisa. Ujumbe wa Sardi, kile kipindi cha matengenezo. Masalia waaminio wachache sana waliosalia, karibu wamalizike.

²⁹ Sasa kwa baadhi ya wageni, huenda nikasema juu ya hili hapa, ya kwamba. . . msije mkaachwa nyuma kwake. Kidogo ni ghafi, na wakati mwingine tutafikia ambapo tunaweza kuweka jumbe zetu kwenye. . . kuuchora, nje alasiri na kuutengeneza; huenda nikafanya hivyo Jumapili. Sasa, kila moja ya hizi zinawakilisha ninii. . . wakati wa kanisa: moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba. *Hiki* kikianza na Filadelfia. . .

³⁰ Na *hiki* hapa juu kinawakilisha ngu—nguvu za kipentekoste, ama kanisa lililokuweco Pentekoste. Lilikuwa ni kanisa kubwa mno hapo mwanzo, bali ro—ro—roho ya kidhehebu ikaanza kuja miongoni mwao, ikijaribu kulifanya Kanisa dhehebu, ambayo iliitwa “Matendo ya Wanikolai.” Mnaweza kunisikia huko nyuma? Naam? Vema. “Matendo ya Wanikolai.” Sasa, halikuwa ni *fundisho* bado. Ndipo tukalichukua Neno na kulifafanua, kwamba “matendo” yalikuwa ni nini, “Unikolai” ulikuwa ni nini. Hilo ni jina la kigeni kwetu, Unikolai, kwa hiyo nilichukua Kiyunani na kulifafanua. Basi *Niko* linamaanisha “kushinda,” ama “kupiga,” ama “kupindua kitu fulani.” Nikolai, *lai* ni kanisa, “walei.” Nikolai, te—tendo lililokuwa likijaribu kuwapindua walei, na kuweka baraka zote. . . na mtu pekee aliyepaswa kuisoma Biblia, yule pekee aliyepaswa kutoa tafsiri yake, angekuwa ni askofu ama kiongozi fulani mkuu wa kanisa.

³¹ Ndipo tunaona, katika wakati wa pili wa kanisa, ingeanza kubana sana. *Hiki* kingali ni Pentekoste; na *hiki* ni dhehebu (d).

³² Sasa, katika wakati wa tatu wa kanisa, Pergamo, Pentekoste ilikuwa karibu imefinywa ikatoka. Lakini mafundisho ya dhehebu, yalitoka kwenye “matendo” *hapa*, yakaendelea hata kwenye “mafundisho” *hapa*. Ndipo kweli walipata, waliolewa papa hapa. Waliolewa! Ninii. . . kundi hili hapa lililokuwa limeyashinda makundi ya kipentekoste.

³³ Sasa jinsi ninavyolisema hilo, ndugu, hiyo ni kweli kabisa. Hiyo ni kulingana na maandiko matakatifu ya historia. Vitabu vya Baraza la Nikea, *Kitabu cha Wafia Imani cha Foxe*, na vitabu vyote mashuhuri vya kale. Nina baadhi ya maandishi ya kale sana yaliyopo. Na kila kimoja. . . Nasema hili pasipo. . . Sisemi

kuwa mimi ni Mpentekoste. Hilo halimaanishi. . . Ninaposema “pentekoste,” hilo halimaanishi dhehebu hili la siku tunayoishi. Hilo lina hatia tu kama hayo mengine. Bali ninamaanisha pentekoste halisi, Roho halisi wa Mungu pamoja na Mafundisho ya asili, pamoja na baraka asilia, pamoja na majina asilia, kikiwa na kila kitu vile vile hasa kilivyoanza hapo mwanzo ama kilivyopitia kote katika Biblia.

³⁴ Sasa, ndipo tunapofikia kwenye wakati *huu*, mnaona umbali ambao Pentekoste inakuja. Mnaweza kuuona vizuri huko nyuma? Mnaweza kuyasoma mlio huko nyuma kabisa? Vema, *huu* hapa unakuja, jana usiku, ule wakati mkuu tuliomo *hapa*, Konstantino, Konstantino, *K-o-n-s*; nitaliweka. Yeye, akiwa ni kafiri, alikuwa. . . aliwasihii hawa Wakristo *hapa* (wale waliokuwa na mafundisho ya Wanikolai) kama wangemwombea apate kushinda vita fulani; vema, yeye atakuwa Mkristo. Mnamo wakati huo alipokuwa vitani, aliota ndoto kwamba anapaswa. . . Kwa msalaba mweupe uliowekwa mbele zake, akasema, “Utashinda kwa *huu*.” Na hiyo ni kweli. Ndipo akaliamsha jeshi lake na kuchora kwenye ngao zao msalaba mweupe, na hapo ndipo palikuwa mahali lilipozaliwa au lilipoanzia shirika la Katoliki, leo, linaloitwa Mashujaa wa Kolumba.

³⁵ Sasa—sasa, Konstantino, kuna. . . huwezi kuokota jambo moja katika historia, kwamba aliongoka. Alikuwa si kitu ila mwanasiasa mpotovu. Alikuwa na wazo niani mwake ku—kuunganisha ufalme wake na kuuimarisha. Kwa hiyo mwenyewe, akiwa ni kafiri, aliabudu sanamu; ndipo akaona ya kwamba mafundisho ya Wanikolai yalikuwa karibu kusukumiwa mahali fulani, kwa hiyo akatumia mbinu ile ile tuliyoona jana usiku.

³⁶ Naye Yesu alibashiri hilo miaka mia tatu na minne kabla halijatukia, ya kwamba angefundisha mafundisho ya Balaamu. Jinsi ambavyo Balaamu aliwadanganya wana wa Israeli, akawafanya wafanye uasherati na—na kutoa. . . kuchukua vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu, kula vitu. Sasa, tunajua ya kwamba “kula vitu hivi vilivyotolewa sadaka kwa sanamu,” ukweli wake, ulikuwa ni kuabudu. Wakiingia, walikuwa wakizisujudu sanamu, wakizirudisha sanamu kwenye kanisa la Kikristo; kama tu vile Balaamu alivyofanya huko nyuma, aliwafanya Israeli wafanye uasherati, kwenda kwenye karamu hii kubwa ya sanamu.

³⁷ Vema, Konstantino alifanya jambo lile lile kwa mbinu yake, naye akaanzisha kanisa. Aliwapa mengi kwenye lile Baraza la Nikea, halafu wao. . . Alifanya majumba me—mengi makubwa aliyokuwa nayo, na kuyageuza haya kuwa makanisa. Ndipo akatengeneza madhabahu makubwa ya marmar, yaliyonakshiwa kwa dhahabu na vito vya thamani. Juu ya hapo akaweka kitu kama kiti cha enzi, ndipo akamfanya mtu mmoja

kiongozi kama. . . alitwa basi “askofu.” Basi wakampandisha kwenye kiti hiki cha enzi, Bonifaso III akatawazwa. Si kwamba tu alitembea huku amevaa mavazi kama—kama mkulima mdogo alivyofanya, bali walimtengenezea ma—majoho makubwa mazuri na kumvalisha kama mungu na kumpandisha pale na kumwita, “Halifa.” Halifa, ama *Vicarivs Filii Dei*, linamaanisha “badala ya Mwana wa Mungu.”

³⁸ Sasa, hili ni kwake aliye na hekima, chora, andika hilo: *Vicarivs Filii Dei*. Ndipo unapochora mstari hapa chini na kuongeza hizo namba, basi utapata kile hasa ambacho Mungu alisema alama ya mnyama ilikuwa: mia sita na sitini na sita. Mnaona, *Vicarivs Filii*. . . Sasa, nimekuwa Rumi na nimekuwa Vatikani. Na ile taji yenye sehemu tatu: mamlaka juu ya kuzimu, mbinguni, na toharani. Mnaona? Nimeiona hiyo taji, nimeiona ile vesti, nikaona yote, papo hapo.

³⁹ Kwa kweli, mnamo Alhamisi alasiri saa tisa nilikusudiwa kukutana na yule papa wa *mwisho* aliyekuwako. Baron Von Blomberg alikuwa na. . . halafu akasema, “Sasa, utakapoenda, Ndugu Branham, jambo la kwanza linalokupasa kufanya ni kupiga magoti kwa goti lako la kuume na kuibusu pete hiyo.”

⁴⁰ Nikasema, “Hilo haliwezekani. Hilo haliwezekani. Lisahau tu.” Nikasema, “Nitatoa. . . sina neno dhidi ya mtu huyo, yeye. . . ? . . .” Lakini nikasema, “Lipo jambo moja, nitampa mtu wadhifa wake. Kama yeye ni ‘Kasisi,’ hilo ni sawa, ‘Askofu, Mzee, Daktari,’ wote ule, nitamsalimia mtu kwa furaha. Bali kumsujudia mtu? Ninawiwa na mtu mmoja tu heshima kuu: Yesu Kristo. Huyo ndiye mtu pekee ningemsujudia.” Nikasema, “Sahau tu. Ifutilie mbali tu.” Nisingeichukua. Na kwa hiyo mimi. . .

⁴¹ Baada ya kufika nyumbani nikakuta kwamba kulikuwako na Mmarekani mwingine mashuhuri aliyefanya hivyo, pia, Teddy Roosevelt. Alikataa kufanya hivyo kwa sababu ya. . . Mnaikumbuka hiyo katika historia? Kwamba alikataa kumwona Papa kwa kuwa ilibidi aibusu pete yake ama. . . Walikuwa wameiweka kwenye kidole gumba, pia, mwajua. Kwa hiyo. . . Loo, la. La, hilo haliwezekani. Kwa hiyo basi. . .

⁴² Hata hivyo, katika. . . Sasa, kama Balaamu. . . Basi tuliona jana usiku, kwenye. . . Sasa, hapa kwanza, kabla hatujaondoka hapa, waliliunganisha kanisa na kufunga ndoa, wakapata mawazo ya kikafiri, sanamu za kikafiri zilizokuwa kanisani. Mungu wa Jupita, mungu wa jua, mungu wa Marsi, mungu wa Venasi, na sanamu hizo zote za miungu naye akazitoa zote kutoka kwenye makanisa ya kikafiri; ndipo akapandisha Paulo, Petro, bikira Mariamu, wote hao, na kusema, “Huyu hapa Halifa wenu kwa sababu Yesu alimwambia Petro, ‘Nakupa funguo,’ naye ni halifa wa kimitume.” Hilo lingali ni fundisho la Katoliki hata wa leo. Nao wakainua sanamu. Nao walifanya nini?

Wakaingiza ibada ya sanamu katika Ukristo, unaoitwa Ukristo; sio Ukristo halisi, kwa sababu maskini hao wapentekoste. . .

⁴³ Sasa kumbukeni, sisemi. . . Sikusema, “Baptisti, Methodisti, Presbiteri,” wako ndani ya zote. Lakini kitu halisi, cha kweli cha Mungu kilikuwa ni pentekoste; kilikuwa, kiko, na daima kitakuwa! Hapo ndipo Kanisa lilipoanzia, papa hapa likiwa na Nguvu za Kipentekoste.

⁴⁴ Sasa, mnasema, “Hiyo ni kweli, Ndugu Branham?” Nitawaomba mchukue historia, na mwangalie kupitia mtiririko wa wakati kufikia hapa, muone kama kila mmoja wa hao watoto wa kweli wa Mungu hawakuishikilia Baraka ya Pentekoste; wakanena kwa lugha, wakafasiri lugha, walikuwa na ishara na maajabu, wakabatiza katika Jina la Yesu Kristo. Kila kitu walichofanya mitume, walikifanya pia, moja kwa moja kupitia kule. Hiyo ndiyo sababu kule ndani, nikisoma historia, nilimchukua Paulo na Ireneo na—na—na—na kote kote kufikia Mtakatifu Martin, Kolumba; kila mmoja wa hao watu (moja kwa moja mpaka kwenye wakati huu hapa), walikuwa na ishara na maajabu.

⁴⁵ Vema. Yeye alisema walikuwa. . . maikrofoni ilikuwa kidogo. . . Hiyo ni afadhali? Vema. La, wanatikisa kichwa chao, hawawezi kusikia hata kidogo sasa, Billy. Vema. Mnaweza. . . ? Ni. . . ? Sasa, mnanisikia sasa? Sasa, na hiyo je? Hiyo ni afadhali? Naam? Kila mtu anasema, “Sawa.” Paulo, hilo ni doa moja dhidi yako. Vema, sawa.

⁴⁶ Sasa, katika wakati huu hapa basi wakati alipokitengeneza kitu hiki kikubwa mno, na kumbandisha mtu huyu hapa kama askofu wa ulimwengu mzima juu ya makanisa yote, akawapa fedha nyingi sana na kadhalika, na kuwaahidi, naye akaliunganisha kanisa pamoja na taifa, na kuliacha kanisa liwe na mamlaka juu ya taifa. Akamfanya mtu mkuu. Kwa hiyo hapo ndipo hasa. . . Kile Konstantino alichofanya ni jambo lile lile tulilopata huku kwenye kanisa hili lingine, kwamba kile Mungu alisema; kwamba, katika siku za Eliya, kwamba walimridhia huyo mwanamke Yezabeli kuwatawala watoto Wake; ambalo lilitukia katika Wakati wa Giza. Basi angalia hapa ambapo Pentekoste ilipo sasa. Jamani, jamani! Ilizimika kabisa. Na kwa yapata miaka elfu moja, ilinini. . . kuanzia mwaka wa 500 hadi 1500, kweli, hiyo ni mwaka wa 606 hadi miaka ya 530. . . ’520, ndizo namba halisi, lakini moja kwa moja kwenye miaka elfu moja. Wataninii. . . mateso ya umwagikaji wa damu. Someni historia.

⁴⁷ Sasa, Mkatoliki atakwambia ya kwamba kanisa la Kikristo, walikuwa ndio kanisa la Kikristo. Hao ni kanisa la *kimadhehebu* la Kikristo. Lakini wapentekoste wa kweli walikandamizwa sana, wakauawa, wakauawa kinyama, na kuuawa na mapapa

na maaskofu na kadhalika, ya umwagikaji wa damu ilivyoweza kuwa.

48 Sasa, siku moja hiyo itanigharimu maisha yangu, mnaona, kusema hilo. Lakini hilo ni jambo moja la hakika, ninajua ninakoelekea, sasa najua. Inaendelea tu kutiririka damu. Bali ile saa inakaribia sasa, ambayo mnaona kulingana na yale yanayoendelea nchini kwamba haitachukua muda mrefu. Kamwe usiighairi Hiyo! Hiyo ni Kweli. Dumu moja kwa moja Nayo. Ichanganye damu yako kama wale wa siku ile.

49 Sasa, humu ndani mnaona lililotukia. Kisha hapa ndani mafundisho ya Yezebeli yanaingia. Yezebeli alikuwa ni mwanamke, kafiri ambaye. . . Ahabu alifanya jambo lile lile ambalo Konstantino alifanya; akamwoa mwanamke huyu kusudi aimarishe ufalme wake, na akaingiza ibada ya sanamu katika Israeli kama tu vile Konstantino alivyofanya huko nyuma. Nayo Pentekoste ilikuwa karibu imekwisha kabisa.

50 Sasa, Mungu alimwinua Martin Luther. Nawatakeni muone jinsi linavyoondoka *hapa* na karibu litoweke kabisa, kisha linaibuka kidogo sana *hapa*, na kushuka kuja *hapa* tena. Nami kidogo nilichora mstari hapo kwa sababu ni—ni somo kuu la Jumapili usiku, Bwana akipenda.

51 Sasa—sasa, ninaamini kidogo tumeshikwa sasa mahali tulipo. Sasa, papa *hapa* ndani ni Wa—Wakati wa Giza, papa hapa, kutoka mwaka wa 1500. . . kutoka mwaka wa 606 hadi 1520. Papa hapa ndani. Nitaweka hili hapa kusudi mtaninii. . . mwaka wa 606 hadi 1520. Huo ni Wakati wa Giza, kanisa hili papa *hapa*, Wakati wa Giza. Sasa, kanisa hili tunaloliendea sasa ni kanisa la Kilutheri.

52 Sasa, karibu kila mmoja kule nyuma, hao watu walikufa huko kwenye. . . Watu hawa kama Ireneo, na Martin, na Kolumba, nao wakatoweka. Na sasa hebu chukua mtu yeyote anayetaka kutafuta historia yoyote mnyotaka, kama ni historia ya kweli, na wanapokwambia ya kwamba “Mtakatifu Patrick alikuwa ni Mkatoliki,” hawajui wanalozungumzia. Mtakatifu Patrick alilipinga kanisa Katoliki, wala kamwe hakwenda Rumi, na aliyakataa mafundisho yao kwa dhati. Hiyo ni kweli kabisa. Ukienda kaskazini mwa Uinge-. . . ama Ayalandi leo, basi utaona kitu kile kile. Mtakatifu Patrick alikuwa ni mtu wa Mungu! Lakini, Mtakatifu Patrick, wakati inaposemwa mle ndani ya kwamba a—aliwafukuza nyoka wote kutoka Ayalandi, hiyo ilikuwa ni hadithi ya uongo.

53 Ni wangapi wenu waliopata kusoma na kusikia habari za William Tell akipiga risasi tofaa kutoka kichwani mwa mvulana wake? Hiyo ni hadithi ya uongo ya Katoliki, hata neno lake moja si kweli. Nilikuwa pale pale ambapo ilisemekana lilitukia. Imeandikwa pale juu, “hadithi ya uongo, si ya kweli,” huko Uswisi. Mimi na Billy tulikuwa tumeketi pale pale kando ya

Ziwa Lucerne ambapo alifanya ja—jambo hilo lilipokuwa, yeye alimpiga mtu risasi; hiyo ni kweli, bali si tofaa juu ya kichwa cha mvulana wake. Hiyo ni hadithi tu ya uongo, ushirikina na kadhalika, kamwe haikuwa hivyo. Hawana taarifa yake kule, mahali lilipotukia wala chochote kile, kwamba alilifanya. Nayo inalielezea waziwazi pale na kusema ilivyokuwa. Sasa, lakini katika hii, hakuna historia halisi inayosema alifanya hilo. Mnaona.

⁵⁴ Kwa hiyo sasa hapa ndani, katika wakati wa kanisa, hapo ndipo karibu lififie kabisa, likaisha lisikuweco tena. Sasa katika wakati huu mwingine anakuja wakati wa Matengenezo. Sasa, mambo haya hapa baada ya karibu miaka elfu moja ya weusi na giza na kufifia kabisa, na kadhalika namna hiyo, kanisa kwa namna fulani halikumwona tena Ireneo. Yeye alikuwa mtu mashuhuri, mtauwa. Vivyo hivyo na mamia ya wengine wa hao watakatifu wa thamani walioimwaga damu yao ya uhai kwa hiari yao (wakisimama kwenye ule uwanja wa michezo) walivyoweza, mnaona, kwa ajili ya huduma ya Kristo, kwa ajili ya ubatizo katika Jina la Yesu Kristo, kwa kunena katika lugha, kufufuka kwa Yesu Kristo akiishi ndani ya maisha hayo na uwepo Wake wa Kiungu hapo, huku watu *wanaojiita* Wakristo wakiwatesa. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli kabisa.

⁵⁵ Loo, ni—ni jeshi la kipepo la wanaostahili kuzimu sijui nini. Wanajitokeza namna hiyo na kujipanga wenyewe na kujifanya, “anajiita nabii mke, mfasiri wa kiungu wa Neno, hakuna alijuaye ila wao.” Anajiita mwenyewe, bali yeye ni mwongo. Mnaona? Hapo mnaona. Lakini wakati uo huo; anaye malaika Wake pale, aliye na Kweli. Ukweli daima utarudi kwenye Hili. Mnaona? Daima utarudi kwenye asili, kwa sababu Mungu kamwe habadiliki kutoka kwa Hilo.

⁵⁶ Sasa, na tuliona pia, jana usiku, kabla hatujaliacha hili, kusudi litatulike moyoni mwenu. Si kwamba tu... Katika mfano, Yezebeli, alikuwa na bi—binti. Mnakumbuka hilo? Nao Ufunuo 13 ulisema kanisa hili kengeufu, Rumi, lilikuwa na mabinti. “Alikuwa ni mama wa makahaba.” Hiyo ni kweli? Yezebeli alikuwa na binti, naye Yezebeli alifanya nini na binti yake? Mnaona jinsi mambo hayo yote, mifano na vivuli. Yezebeli alihakikisha kwamba binti yake ataolewa na Yehoram, ambaye alikuwa ni mwana wa Yehoshafati katika Uyahudi.

⁵⁷ Israeli ilikuwa imegawanyika wakati huo, namna hii. Hii *hapa* Yerusalemu, na huu *hapa* Uyahudi. Vema, Ahabu alikuwa *hapa*, naye Yehoram alikuwa *hapa*. Vema, Yezebeli alikuwa ameishinda *hii*, Israeli yote ilichukua sanamu. Ndipo... (Wote ila Eliya na hilo kundi dogo aminifu.) Vema. Sasa, upande *huu* walikuwa ni Yehoram juu ya Yuda; na wakati alipomzaa mtoto na Ahabu, alimchukua msichana huyu na kumwoza kwa mwana wa Yehoram... ama mwana wa Yehoshafati ambaye alikuwa

ni Yehoram, ndipo akaingiza ibada ya sanamu katika Yuda, na kujenga madhabahu ya kipagani Yerusalemu.

⁵⁸ Hivyo ndivyo kanisa Katoliki lilivyofanya hasa! Liliyabandika mafundisho yake ya kimadhehebu na kadhalika, na kumkatilia mbali Roho Mtakatifu kutoka kanisani *hapa* chini pamoja na binti yake (Lutheri, Methodisti, Baptisti, Pentekoste, na kadhalika). Hivyo ndivyo alivyofanya hasa. Biblia ilisema, “Yeye ni mama wa makahaba.”

⁵⁹ Sasa, hebu angalia tu kote katika Maandiko. Ukiona—ukiona kitu chochote tofauti katika Maandiko, na historia ikipiga shabaha zizo hizo, wewe njoo kwangu kama muungwana. Unaona? Hiyo ni kweli. Hakipo!

⁶⁰ Haya madhehebu ndiyo vitu vyenye sumu tulivyowahi kuwa navyo katika Uprotestanti, kujaribu kuwafanya wanadamu walitawale kanisa, sanamu nyingine kama ile iliyoketi kwenye kiti cha enzi. Askofu mkuu, wasimamizi wakuu wa Kipentekoste, “Vema, sasa, hebu nione, fundisho lake ni gani? Loo, yeye alibatiza katika Jina la Yesu? Hawezi kuja kwenye hili. La, bwana, ndugu. Msiukubali.” Na hilo limekataliwa, pia. “Nataka mnielewe, asije yeyote wenu akahudhuria mkutano huo huko. Umekataliwa. Haijalishi wewe ni mgonjwa jinsi gani, kaa mbali nao, haijalishi Mungu anafanya nini. Kama huangalii kupitia kwa miwani yetu, mbona, huoni hata kidogo.” Wakawa na sanamu ya mnyama! Nayo sanamu hiyo ilikuwa na uhai wa kunena. Ni kweli kabisa. Ati hufikiri kwamba anaweza kunena, hebu mkasirishe kidogo wakati mmoja. Uh-huh, hakika unaweza kuingia matatani.

⁶¹ Ninakumbuka, huko Tulsa, Oklahoma, nilikuwa . . . Loo, nilikuwa nikiingia katika machafuko mabaya sana kule, hayo madhehebu yakaanza kuyumbayumba kule. Nilikuwa nimeketi katika hili jengo siku moja ndipo nikaona o—ono. Niliona na—nani mdogo . . . maskini mtoto mdogo wa paka, naye alikuwa amelalia mto wa hariri, naye alikuwa ni jamaa mdogo mwenye sura nzuri sana. Nami nikaenda pale (nami namwogopa paka), basi nikaenda pale na kuanza kumpapasapapasa, naye alikuwa akifanya, “purr, purr.” Mnajua jinsi wanavyotoa hiyo sauti ya kuchekesha, mwajua. Nami nilikuwa nikimpapasa, nikasema, “Maskini kitoto cha paka cha kupendeza.” Naye akasema, “purr,” vizuri tu, mwajua.

⁶² Ndipo nikaangalia nyuma ya mto wake, pameandikwa, “Kijipaka cha Kipentekoste.” Vema, nikawazia, “Sasa, hiyo si ni ajabu.” Nami nikasema, “Hili halina budi kuwa ni ono.”

⁶³ Ndipo kitu Fulani kikasema, “Mradi tu unapapasa manyoya yake hivi, yote ni sawa; lakini sasa kama unataka kuona yeye ameundwa na nini, kwaruza manyoya yake kinyumenyume.” Mnaona? Kwa hiyo nilipoyakwaruza—kwaruza manyoya yake kinyumenyume, macho hayo yakatokeza, chanikiwiti, naye

alikuwa ni mnyama mkali amesimama hapo akinitemea mate kwa nguvu alivyoweza. Mnaona, kwaruza tu manyoya yake kinyumenyume kidogo. Hebu mwambie ubatizo wake katika “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu” ni wa ibilisi na ni wa kanisa Katoliki, uangalie kile kitakachompata. Unaona? Manyoya yake yanasimama.

⁶⁴ Nikashuka kuja, nikamwambia Ndugu Gene na hao wengine, huko chini katika . . . loo, Ndugu Leo na hao wengine, nikasema, “Hakika niliona ono halisi la madhehebu ya Kipentekoste katika hili.”

⁶⁵ Sasa mlango wa 3, hebu kwanza . . . Sardi ni kanisa lililokufa. Limekufa kwa sababu waliuawa kwenye wakati huu. Ni kamba ndogo tu ya Uhai, tutaona katika dakika chache kwamba ilikuwa ni kitu gani, katika muda mfupi tu. Kuanzia mwaka wa 1520 hadi 1750 ilikuwa ni Wakati huu wa Sardi. Nayoya nyota, ama malaika wa . . . Nyota iliyokuwa mkononi Mwake, ambayo ilikuwa ni malaika ama mjumbe wa wakati huo wa kanisa. Hilo limeeleweka dhahiri? Kwamba nyota ilikuwa ni malaika, naye malaika ni mjumbe wa wakati huo. Vema. Vema.

⁶⁶ Sasa tumemaliza na Baraza la Nikea. Lilikufia huko nyuma, nao wote wakaingia katika mamlaka na utukufu, kanisa na taifa wakaungana. Basi mtu yeyote anaweza kukumbuka vile someo lilivyosema jana usiku, vile wengi wa watu hao walivyowazia? “Utawala wa Miaka Elfu ulikuwa umeanza.” Na ninii yote . . . “Kuingiza Utawala wa Miaka Elfu pasipo na kuja kwa Kristo.” Mnaona? Kuja kwa Kristo kunauanzisha Utawala wa Miaka Elfu, jambo la kwanza. Na katika siku hizo walikuwa na . . . Kama ukiichukua historia, utaona walikuwa na Mayesu wa uongo walioinuka na kadhalika, mnaona. Na hata walidhani ya kwamba papa alikuwa ni Yesu, huku wakimwita *halifa*, “badala ya Mwana wa Mungu.” Naam, kama, mungu mkubwa mtakatifu, ameketi pale.

⁶⁷ Hebu niwaambieni jambo fulani. Biblia inasema ya kwamba Yesu atakapokuja . . . kabla hajaja, “Watainuka manabii wa uongo, na watainuka Ma-Yesu wa uongo.” Hiyo ni kweli. “Lo, hapa . . .” Lakini hebu niingize tu hili moyoni mwako: kamwe hapatakuwako na Yesu yeyote atakayeweka mguu Wake juu ya hii nchi mpaka Kanisa limekwisha kunyakuliwa na kuondoka. Sasa, liwekeni tu hilo niani mwenu, kwa maana kutakuwako na makristo wa uongo watakaoinuka. Bali Yesu hatakuwa hapa duniani; maana parapanda Italia, na Yeye haji, tunamlaki hewani. Kanisa tayari limeondoka. Ndipo basi wakati Yesu atakapotokea, itakuwa ni kule kurudi. Mataifa yanaenda kumlaki hewani. Hayo ni Maandiko? Mnaona? Wanaenda kumlaki hewani, ndipo twende juu. Naye Yesu ni . . . kamwe hakanyagi ardhini mpaka Kanisa limekwisha kunyakuliwa na kupelekwa Nyumbani na kwenye Karamu ya Arusi huko Mbinguni; ndipo anayarudia masalia ya Wayahudi.

68 Kwa hiyo sasa lilikuwa limemalizika, Baraza la Nikea, kanisa lilikuwa—lilikuwa chini ya utawala wa papa kwa karibu miaka elfu moja. Walikuwa wamewaua wote ambao waliwapinga. Hiyo ni kweli. Ama unakuja chini ya hilo au uli—uli—uliuawa, kama vile Yezebeli alivyoifanyia Israeli.

69 Kwa jumla Roho Mtakatifu alikuwa amewaacha isipokuwa tu wachache sana kwenye wakati huu, kama vile Eliya na masalia wa Israeli ambao hawakuwa wamempigia Balaamu goti. Kama ungetaka kusoma hayo pale chini, hiyo ni Wafalme wa Kwanza, mlango wa 19, na kifungu cha 18, wakati Eliya alipokuwa amesimama huko nyuma pangoni na akasema, “Bwana, wa—wamewaua manabii wako wote. Wamefanya kila kitu, na mimi—mimi niko peke yangu. Nami ndimi tu niliyesalia.” Lakini Mungu akamwambia alikuwa na mamia kadhaa bado ambao hawakuwa wamempigia Baali goti, kwenye walei huko nje.

70 Na kwa hiyo, Sardi, sasa tunaanza. Neno lenyewe *Sardi*, kifungu cha kwanza. Neno *Sardi*, katika msamiati wa Kiingereza, linamaanisha, kama unataka kulichunguza, linamaanisha “walioponyoka.” *Sardi* wa kweli walikuwa ni “wale walioponyoka.” Hivyo ndivyo *Sardi* linavyoamaanisha, vema, “walioponyoka.” Sasa, mnaona, na “walioponyoka.”

71 Sasa tutaanza kwenye cha kwanza. Wenyewe... Tutauita *wakati wa Matengenezo* na ni jambo linalofaa sana kwa matengenezo haya kama tutauita hivyo, kwa sababu ni... Matengenezo yalikuwa ni “walioponyoka” ambao walitoka na kuponyoka kutoka kwake.

72 Sasa hebu tukichukue kifungu cha kwanza:

...kwa malaika wa kanisa lililoko Sardi andika; Haya ndiyo anenayo yeye aliye na...Roho saba za Mungu, na zile nyota saba. Nayajua matendo yako, ya kuwa una jina la kuwa hai, nawe umekufa.

73 Sasa salamu. Sasa, zile Roho saba ni... “Zile Roho saba na nyota saba.” Hizo Roho zilikuwa ni malaika waliokwenda kwenye zile nyota ambazo zilikuwa ni wajumbe. “Roho saba,” mara saba mbalimali Roho Mtakatifu angemia mafuta mjumbe, ambaye alikuwa ni nyota katika siku yake. Ro—Roho ni wa Milele, nayo nyota iliyofanywa kwa kusudi kuakisi Nuru kwenye giza la nyakati hizi za kanisa ambapo taa na nyota zinawakilisha. Malaika, Roho, alikuwa ndiye aliyeenda kwenye nyota na kuiakisi Nuru ya Roho Mtakatifu kupitia kwa nyota hii ya wakati huo wa kanisa. Hilo, mpate kujua... nashangaa hizo Roho saba zilikuwa ni nani. Ni wale wajumbe saba wa zile nyakati saba za kanisa. Mnaona? Sasa, na kila wakati nyota ilipojitokeza jukwaani, Roho Mtakatifu alishuka na kuitia mafuta nyota hiyo na kuiweka kama tu ile ya kwanza ilivyokuwa.

⁷⁴ Sasa hebu—hebu niwathibitishie hilo. Paulo alisema, kama ukitaka kujua ilikuwa ni nyota ya aina gani. Kwa sababu, kumbuka, Shetani ni nyota, pia, nyota ya asubuhi. Sasa angalieni, Paulo alisema. . . Je, mnaamini yeye alikuwa ndiye nyota ya kanisa la Efeso? Yeye alisema, sasa, kama unataka kujua kama ni kweli ama si kweli. Katika Wagalatia 1:8, Paulo alisema, akinena pale, ya kwamba baada ya wakati kuja, na mbwa mwitu wakali na kadhalika, alisema, “Kama malaika akishuka kutoka mbinguni na kufundisha injili nyingine yoyote. . .” (Sasa, yeye alijua mtu huyu alikuwa anakuja aliyeonekana kama malaika na *halifa* mkubwa.) Akasema, “Haidhuru ni nani, kama malaika ama mtu yeyote akija kwenu na kufundisha jambo lingine lolote mbali na hii Injili tuliyoufundisha, na alaaniwe.” Hiyo ni kweli?

⁷⁵ Paulo ndiye aliyewashurutisha kubatizwa tena kama hawakuwa wamebatizwa katika Jina la Yesu Kristo, “Njoni mkabatizwe tena kusudi mumpokee Roho Mtakatifu,” Matendo 19:5. Yeye alikuwa ndiye pia aliyeweka mikono juu ya watu, na karama, na kuliweka kanisa katika utaratibu pamoja na kufanya miujiza, uponyaji wa Kiungu, karama za lugha, kufasiri lugha. Hiyo ni kweli? Wakorintho wa Kwanza 12, muone yale aliyosema Paulo. Wakorintho wa Kwanza 12, nanyi mtalipata. Aliweka kanisani. . . Mungu aliweka kanisani karama hizi kubwa; Paulo alizipangilia, na kuziweka katika utaratibu zipate kutenda kazi kwa utukufu wa Mungu. Paulo alisema hivyo. Basi kama mtu yeyote, haidhuru yeye ni wa dhehebu gani, anayejaribu kuwaambia ya kwamba siku za kunena kwa lugha, kufasiriwa kwa lugha, uponyaji wa Kiungu, na miujiza, na ushuhuda wa Roho Mtakatifu kama ubatizo. . . na alaaniwe. Kwa maana Roho yeye yule aliyekuwa juu ya Paulo atakuwa ni Roho yeye yule aliyetumwa kwenye wakati huo mwingine wa kanisa, yule yule kwa wakati huo mwingine wa kanisa, na yule yule hata mwisho wa wakati wa kanisa. Roho yule yule, Roho Mtakatifu. Mnaamini hilo?

⁷⁶ Kama ukiangalia hili, hili limeandikwa hapa. Mwandishi alijua. Angalieni, “Roho saba.” Angalia: herufi kubwa “R,” Roho Mtakatifu, ni mmoja tu. Uh-huh. Roho Mtakatifu yule yule akija mara saba kwenye nyakati zote za kanisa akiwa na Nuru ile ile. Mnalipata sasa? Nyakati saba za kanisa, mara saba huyu Roho Mtakatifu angeubeba Ujumbe uu huu! Ambao ulitangaziwa laana kwa mtu yeyote ambaye angeubadilisha.

⁷⁷ Sasa angalia kama hilo linaafikiana na ufunuo wa kitu hicho chote. Yeye alisema, “Kila atakayeondoa au kuongeza kwake, huyo ataondolewa (sehemu yake) kutoka kwenye Kitabu cha Uzima.” Hicho ni kitu hicho chote kufunikwa basi. Kwa hiyo hakuna nafasi kwako kuruka ama kujibania mahali pengine popote, unaona, maana Hilo ndilo. Hivyo ndivyo Mungu alivyosema, hivyo ndivyo Roho alivyosema, na

hivyo ndivyo Makanisa yalivyosema. Sasa, kama ukijaribu kulazimisha namna nyingine yoyote ya fundisho mbali na lile Paulo alilofundisha, ni makosa! Biblia ni sahihi. Maisha yake . . . Yesu alisema, “Nitamwondolea sehemu yake katika Kitabu cha Uzima.”

78 Sasa, mnasema, “Sehemu gani ya Kitabu cha Uzima?”

79 Wapo watu wengi walio na majina yao katika Kitabu cha Uzima ambao hakika watashindwa. Mnajua hilo, sivyo? Mnakumbuka yale mafundisho hivi majuzi usiku? Mliyapata? Huenda tukayapitia hayo; haisikiki ni nzuri bado; haionekani kuwa sawa, mnaona.

80 Yuda Iskariote alikuwa mwana wa Shetani, alikuwa ni ibilisi aliyedhihirishwa katika mwili. Biblia ilisema alikuwa hivyo. Biblia ilisema, “Alizaliwa mwana wa upotevu.”

81 Angalieni hili kwa dakika moja tu. Sasa, kwenye *huyu* alikuwako Yesu; huyu *hapa* mwizi mkono Wake wa kulia; huyu *hapa* alikuwa mmoja mkono Wake wa kushoto. Sasa, wakati . . . Yesu alikuwa ni Mwana wa Mungu. Hiyo ni kweli? Sasa, watu wengine huona tu misalaba mitatu, bali kulikuwako minne. Misalaba minne! Sasa, msalaba ni kitu gani? Ni mti. Hiyo ni kweli? Biblia ilisema, “Amelaaniwa kila mtu aangikwaye juu ya mti.” Naye alifanywa laana kwa ajili yetu, aliangikwa mtini. Ulikuwa umekatwa ukaanguka, bali ulikuwa mti. Hiyo ni kweli? Vema. *Hapa* chini, chini ya kilima, ulisimama mwingine. Yuda alijinyonga juu ya mkuyu. Hiyo ni kweli?

82 Angalieni! Huyu *hapa* Mwana wa Mungu; alitoka Mbinguni, anarudi Mbinguni, akichukua pamoja Naye mwenye dhambi aliyetubu. Huyu *hapa* mwana wa upotevu; alitoka kuzimu, anarudi kuzimu, akichukua pamoja naye (“Ikiwa Wewe ni!”) mwenye dhambi asiyetubu. Mnaona, mwenye dhambi asiyetubu, “Ikiwa Wewe ni Mwana wa Mungu, jiokoe Mwenyewe pamoja na sisi pia.”

83 *Huyu* alisema, “Tuna . . .” (kuhubiri, yule mhubiri wa Injili) “Tunastahili kile tunachopata, lakini mtu huyu hajafanya chochote. Bwana, nikumbuke utakapokuja katika Ufalme Wako.” Huyu alikuwa ni nani?

84 Ilikuwa . . . ? . . . kidogo jana usiku ama usiku uliotangulia. *Huyu* ni Habili wa Mungu; *huyu* ni Kaini wa ibilisi. Kama vile Kaini alivyomwua Habili madhabahuni, Yuda alimwua Yesu madhabahuni. Hiyo ni kweli. Moshi unapanda tu juu *huko* nyuma sana katika Edeni na unatulia papa *hapa* tena. Hiyo ni hakika.

85 Loo, ni tukufu, barabara ile ya kale, barabara ya kale iliyobarikiwa, iliyojaa tu utukufu.

⁸⁶ Sasa, sasa tunaona hapa (Samahani.) ya kwamba kanisa hili la Sardi, kwa malaika, Yeye alisema, “Hizo Roho saba; Yeye aliye na hizo Roho saba.”

*...kwa malaika wa kanisa lililoko Sardi andika;
Haya ndiyo anenayo yeye aliye na hizo Roho saba za
Mungu,...*

⁸⁷ Na sasa ni wangapi wanaojua ya kwamba Mungu ni Roho mmoja? Hakika. Mungu, Roho Mtakatifu. Mungu, Baba, Roho Mtakatifu, wote ni Mtu yule yule, maana Mariamu alikuwa na mimba ya Roho Mtakatifu. Sasa, ninii... bali Mungu alimtumia huyu Roho Mtakatifu katika Nuru saba mbalimbali za kiinjilisti kwa Kanisa, nyakati saba za kanisa. Mnalipata? Nyakati saba za kanisa.

⁸⁸ Sasa, mnasema, “Mungu hafanyi hivyo.” Loo, naam, ndugu.

⁸⁹ Angalia! Yeye alitumia Roho ya Eliya, na wakati Elisha alipoondoka... Eliya alipoondoka, Elisha alipokea sehemu maradufu Yake. Ndipo Elisha aliposhikwa na ugonjwa akafa, ndipo ilirudi tena juu ya Yohana Mbatizaji. Kitu kile kile, kikamfanya atende kama tu Eliya alivyotenda, kuishi nyikani na kadhalika. Hiyo ni kweli? Nayo imebashiriwa kuja tena katika siku za mwisho, mnaona. Mungu anamtumia Roho huyo kote kote.

⁹⁰ Naye Yesu alitiwa mafuta kwa Roho Mtakatifu, akazunguka huku na huku akitenda wema. Hiyo ni kweli? Naye Roho Mtakatifu yule yule aliyekuwa juu ya Yesu, alirudi moja kwa moja Kanisani kwenye Siku ya Pentekoste, anarudi moja kwa moja kwenye wakati unaofuata, wakati unaofuata, wakati unaofuata. Basi ni kitu gani? Roho Mtakatifu mmoja na yeye yule. Loo, hivi hamwoni? Mungu juu yetu, katika Baba; Mungu pamoja nasi, katika Mwana; Mungu ndani yetu, katika Roho Mtakatifu. Ni ofisi tatu, wala si miungu watatu. Mnaona? Na sifa hizo tatu (Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu) ni za Jina moja: Yesu Kristo. Vema.

⁹¹ Sasa, angalieni sasa tunapoendelea. “Zile Roho saba,” asema Yeye anayeshikilia... Kwa maneno mengine, “anawashika wajumbe Wake.” Wajumbe watakaotiwa mafuta kwa Roho Mtakatifu, kwa Roho Mtakatifu yule yule ambaye Paulo (yule wa kwanza) aliyetiwa mafuta naye, wa pili, wa tatu, wa nne, wa tano, wa sita, na wa saba, wote wako kwenye mkono Wake wa kulia. Loo, wakitoa nguvu zao na Nuru yao kutoka kwenye mkono Wake wa kulia.

⁹² Sasa, Yeye alipaa Juu. Naye Filipino akasema, wakati alipokuwa akifa... Ama Stefano alisema, “Naona mbingu zimefunguka, na... na Yesu ameketi mkono wa kulia wa Mungu.” Hiyo haimaanishi ya kwamba Mungu ana mkono mkubwa mno wa kulia na Yeye ameketi juu yake, bali *mkono wa kulia* unamaanisha mkono wa kulia wa “nguvu na mamlaka.”

⁹³ Mwili huo ambao Mungu aliumba...“Sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu, wala sitaiacha nafsi Yake katika kuzimu, bali nilimfufua na kumweka badala ya Roho juu ya madhabahu.” Angalieni! Wakati walipomwona Yeye—Yeye ameketi madhabahuni, na alikuwa na Kitabu mkononi Mwake, na hakuna mtu aliye juu ya nchi wala chini ya nchi, wala popote pale, aliyeweza ama aliyestahili hata kukiangalia hicho Kitabu; bali Mwana-kondoo ambaye kana kwamba alikuwa amechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, huko nyuma kabisa mwanzoni wakati Yeye alipowazia juu ya mwili huu uliokombolewa kwa mara ya kwanza, alikuja akakichukua kutoka mkono wa Yeye aketiye juu ya Kiti cha Enzi, kisha akaketi, Mwenyewe. Amina. Haya basi. Haya ni Maandiko. Ni mazuri tu, mnaona.

⁹⁴ Sasa, “Yeye ashindaye ataketi pamoja Nami juu ya Kiti Changu cha Enzi, kama Mimi nilivyoshinda na kuketi kwenye Kiti cha Enzi cha Baba Yangu.” Kwa maneno mengine, “Nilichukua ndani ya mwili Wangu Roho Mtakatifu. Nilishinda mambo yote ya ulimwengu (kupitia majaribu) kwa Roho Mtakatifu, na kuchukua mamlaka!” (“Na ndani Yake mnakaa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili.”) “Nimepewa mamlaka yote Mbinguni na duniani mikononi Mwangu,” akasema. Mamlaka yote! Basi Mungu hana mamlaka kama Yeye ni mtu mwingine. Kwa kuwa Biblia ilisema, Yesu alisema, baada ya kufufuka Kwake, ya kwamba “Mamlaka yote Mbinguni na duniani, pia, yaliwekwa mkononi Mwangu.”

⁹⁵ Naye Yesu anakuja kutoka Mbinguni pamoja na elfu kumi mara elfu kumi ya Watakatifu Wake, nayo Biblia inasema ya kwamba “Mbingu ilikuwa tupu kwa muda wa nusu saa.” Yuko wapi jamaa huyu mkubwa, Mungu, basi? Uh-huh. Mnaona? Yuko ndani ya Kristo. Hakika! Na tunaposhinda kwa Roho Mtakatifu kama vile alivyofanya, tutaketi pamoja na Yeye wakati akichukua kiti cha enzi cha duniani cha Daudi, tuketi na kutawala pamoja Naye kama tu Yeye alivyofanya huko Juu, (Amina!) pamoja na uwezo na mamlaka juu ya dunia nzima. “Nao ni. . . dunia inaugua, ikingojea madhihirisho ya wana wa Mungu wapate kudhihirishwa, mwana wa Mungu.”

⁹⁶ Kwa sababu, hata hivyo, ulimwengu huu haukutolewa upate kutawaliwa na Mungu. Hebu tuone kwamba hiyo ni kweli. Mungu wa dunia hii ni nani? Mwanadamu! Hiyo ndiyo milki yake. Wote, kila kitu duniani kinatawaliwa na mwanadamu. Kupitia kwa dhambi alianguka; kupitia kwa nguvu za Kristo za ukombozi anarudi tena. Hiyo ni kweli, kwa sababu dunia ni mali ya mwanadamu, alipewa naye alikuwa mtawala juu ya kila kitu. Na viumbe vyote vinaugua, vikingojea wakati huo ambapo wana wa Mungu watadhihirishwa tena. Loo, mie; loo, jamani! Madhihirisho ya wana wa Mungu. Sasa, afadhali tuliache hilo sasa hivi.

⁹⁷ Lakini, hao wajumbe wako kwenye mkono Wake wa kulia, wakingojea. Popote anapowatuma, watasema kitu kile kile. Kwa kuwa Roho Mtakatifu aliyekuwa ndani ya Kristo... Loo! Roho aliyekuwa ndani ya Kristo! Wakati alipoondoka, Yeye alisema, “Bado kitambo kidogo na ulimwengu...” (*kosmos*, neno la kiyunani ambalo linamaamisha ‘utaratibu wa ulimwengu’; sio dunia, ulimwengu, utaratibu wa ulimwengu) “...hawataniona Mimi tena...” (madhehebu, ama chochote kile) “...hawataniona Mimi tena. Hata hivyo ninyi mtaniona Mimi...” (Kanisa, mwaminio) “...kwa kuwa Mimi...” (“Mimi,” kiwakilishi nafsi ni kweli) “...nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari.” “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” Mnaliona?

⁹⁸ Basi kama huyo alikuwa ni Roho Mtakatifu wa Kristo aliyekuja kwenye Siku ya Pentekoste aliyefanya mambo hayo, ni Roho Mtakatifu wa Kristo ndiye aliyesukumwa *hapa* nje, Roho Mtakatifu wa Kristo angali anashikilia *hapa* ndani, Roho Mtakatifu wa Kristo angali anashikilia *hapa*, *hapa* chini mpaka mwisho wa ulimwengu. Roho Mtakatifu yule yule aliyemjaza Paulo kwa Roho Mtakatifu na mambo aliyofanya, atamjaza *huyu* (Ireneo) ajae Roho Mtakatifu, amjaze Martin ajae Roho Mtakatifu, awajaze hawa wengine wajae Roho Mtakatifu, na alinjaza mimi na wewe tukajaa Roho Mtakatifu, na ni Baraka za Kipentekoste kutoka kwenye kanisa moja hadi lingine; Alfa na Omega, Mwisho na Mwanzo, na Yote, Shina na Mzao wa Daudi, Nyota ya Asubuhi, Ua la Uwandani, Nyinyoro ya Mabondeni, chochote zaidi, Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, Aliyekuwako, Aliyeko, na Atakayekuja, Alfa, Omega, Yote, Yote kwa Yote! Loo, jamani! Hilo lingenifanya kuimba wimbo:

Loo, ati mnasema Mimi ni nani, (kasema Yesu)
ati mlisema nilitoka wapi,

Je, mnajua Baba Yangu, ama mwaweza kujua
Jina Lake?

Yeye alisema: Mimi ni Alfa na Omega, mwanzo
kutoka mwisho,

MIMI NDIMI uumbaji wote, na Yesu ndilo
Jina.

MIMI NDIMI niliyenena na Musa katika
kichaka kilichowaka moto,

MIMI NDIMI Mungu wa Ibrahimu, Nyota ya
Asubuhi Ing’ aayo. (Hiyo ni kweli.)

MIMI NDIMI Ua la Uwandani, basi mlisema
nilitoka wapi?

MIMI NDIMI uumbaji wote, bali Yesu ndilo
Jina.

⁹⁹ Familia yote Mbinguni na duniani inaunganika katika Jina hilo moja (la kote ulimwenguni, lililobarikiwa, likajazwa na Roho Mtakatifu, likaruka chini, likatajwa na Roho Mtakatifu,

likanenwa na Roho Mtakatifu, likazaliwa na Roho Mtakatifu) Jina. Hiyo ni kweli. Mungu aliipa Hilo familia yote ya Mbinguni na duniani. Na kila kitu ndani yake, kila goti, litapigwa kwa Jina hilo. “Wala hakuna Jina lingine chini ya Mbingu walilopewa wanadamu ambalo hatuna budi kuokolewa.” Si *labda*, *tunapaswa*, bali *hatuna budi* kuokolewa. Loo, ninalipenda. Ni zuri tu. Vema.

¹⁰⁰ “Katika mkono Wake wa kulia.” Sasa mnalipata? Ni Kanisa la kipentekoste; uweza, ishara, maajabu yakifanywa kote kote njiani. Sasa sisi ni. . . Tulishuka tukapitia kwenye Wakati wa Giza ambamo lilikuwa karibu kuzimika. Sasa hebu tukichukue kifungu hiki cha 2. Loo, ninaamini tutaendelea tu ki—kidogo na hiki cha kwanza bado:

. . . *nayajua matendo yako, ya kuwa una jina la kuwa hai, nawe umekufa.*

¹⁰¹ Fungueni kwenye kanisa hili lingine hapa, mtaona, “Wala hujalikana jina langu.” Kanisa lifuatalo, “Hukulikana jina langu.” Lakini katika kanisa *hili*, “*Una* jina.” Angalieni hapa! Kanisa *hili* lilitunza Jina Lake; kanisa *hili* lililitunza Jina Lake; kanisa *hili* lililitunza Jina Lake; na kanisa *hili* likapitia kwenye Wakati wa Giza wala hakuna kitu kilichosemwa juu yake; wakati walipotokea kwenye Uzima upande *huu*, wale wa kwanza wachache walioponyoka, wakati Luther alipowatoa, “Una jina la kuwa u hai, bali umekufa.” Sasa, walitumia jina gani baada ya kuacha kuitumia Jina la Yesu? Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Wala hakuna kitu kama hicho. Limekufa—ni theolojia iliyokufa.

¹⁰² Niambieni, je, Baba ni jina? Ni baba wangapi walio hapa ndani? Inua mkono wako. Ni nani kati yenu jina lake ni Baba? Wana? Na wanadamu, hivyo—hivyo ndivyo ilivyo. Sio. . . Jina Lake si Roho Mtakatifu, hivyo ndivyo alivyo; Yeye *ni* Roho Mtakatifu. Jina. . . Roho Mtakatifu si jina, Roho Mtakatifu ni sifa; Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.

¹⁰³ Kwa hiyo mnaona pale, haina msingi tu kama uwana wa Milele ulivyo. Hakuna kitu kama uwana wa Milele. Mwana huzaliwa; Milele kamwe haikuanza.

¹⁰⁴ Hakuna kitu kama hicho, kama nilivyosema hivi majuzi usiku, kama kuzimu ya Milele. Unapataje kuzimu ya Milele kamwe? Kuzimu ilikuwako daima, basi. Biblia ilisema, “Iliumbiwa ibilisi na malaika zake.” Daima kungekuwako na kuzimu; kama daima kutakuwa na moja, ingalibidi kuweko na moja hapo mwanzo. Na kile. . . Ni nani aliyeitumia huko nyuma wakati—wakati Yeye alipokuwa *El*, *Elah*, *Elohimu*, “anayeishi peke Yake,” wakati hakuna kitu kingine? Basi kuzimu ilibidi iwe papo hapo pamoja Naye. Mnaona? “Kuzimu iliumbwa kwa ajili ya ibilisi na malaika zake. Na waovu wote watatupwa ndani yake.” Hiyo ni kweli kabisa. Wataadhibiwa kwa labda miaka milioni mia moja kwa yale waliyofanya. Lakini utakuja

wakati ambapo watakuwa na mauti ya pili. Hakutakuwako na kitu kilichosalia kwao. Kila kitu kilichokuwa na mwanzo kina mwisho. Kwa hiyo tunapoupokea Uzima wa Milele, tunapokea sehemu ya hiyo nurulimwengu ambayo ilikuwa huko nyuma kabla hapajakuwapo na molekuli. Uh-huh. Hiyo Nuru ya Mungu huingia moyoni mwetu ambayo hutuangazia hata tunamwona Yesu. Biblia ilisema, “Hatuoni mambo yote, bali tunamwona Yesu.”

¹⁰⁵ Sasa, Yeye alisema, “Ninajua ni nani. . . Mimi Ndimi niliye na zile Roho saba zinazotumwa kwa yale makanisa saba. Ninajua kazi zako zote na yote kuzihusu, bali una jina ya kwamba u hai bali umekufa.” Sasa, kumbukeni; wakati huu ulikuwa ni wa nani? Martin Luther, wakati wa Kilutheri. Sasa, walihukumwiwa hapo mwanzo. Hata haikuwabidi kuanza, walikuwa wamekufa kwa kuanzia. Haikuwabidi kufa, walikuwa tayari wamekufa. Mnaona, “waliponyoka” tu.

¹⁰⁶ Sasa angalieni hili. Sasa hebu tusome kifungu kinachofuata:

Kukesh! *Uwe mwenye kukesh, ukayaimarisha mambo yaliyosalia, yanayotaka kufa: maana sikuona matendo yako kuwa yametimilika mbele za Mungu.*

¹⁰⁷ Sasa, yeye anazungumza na Luther sasa. Sote tunakubali ya kwamba huu—huu ulikuwa ni wakati wa Luther, ambao ulikuwa ni wa yale matengenezo. Sasa Yeye alisema nini? “Ulileta jina la uongo kwamba u ‘hai,’ bali umekufa.” Walifanya nini? Walilirudisha moja kwa moja katika dhehebu tena. Basi, “nyani haoni ‘kundule,’” msipayuke-payuke, “Katoliki!” Mnaona, maana mmerudi moja kwa moja ndani yake, mkitumia kanuni zake zile zile za imani na majina. Na, vema, Luther alitoa nyingi za katekismo na kadhalika ambavyo kanisa Katoliki lilikuwa navyo, na wakajitwalia jina wenyewe. Mnaona, “Una jina ya kuwa u ‘hai,’ ambao mmetoka kutoka kwenye miaka hii elfu moja iliyokufa hapa, nanyi mngali mnalishikilia hilo jina.” “Una jina,” mnakumbuka?

¹⁰⁸ Kuhakikisha hiyo ni kweli, hayo makanika mengine, yalisema, “Mmelitunza Jina Langu.” “Mmelitunza Jina Langu.” Katika wakati huu “walilipoteza.” Naye anakuja hapa nje na kusema, “Una jina lingine ya kuwa u ‘hai,’ nawe umekufa.”

¹⁰⁹ Loo, ninyi Wamethodisti, Wabaptisti, Presbiteri, Walutheri, na Pentekoste, tubuni mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu. Mnaona? Ondokeni kwenye kanuni hizo za imani zilizokufa na kadhalika ambazo ni za kanisa Katoliki ambalo litaangamizwa na binti zake wote pamoja naye.

¹¹⁰ Hakuna mtu anayeweza kusema kwamba “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,” hizo namna ya . . . Na kitu hicho, nao wanakiita “Utatu Mtakatifu.” Utatu? Ninataka mtu fulani apate hata neno *utatu* katika Biblia, na aje aniambie habari zake, litafute tu neno *utatu*. Hata haliko huko ndani. Hakuna kitu kama hicho.

111 Sasa, sasa:

. . . nayo *yanataka kufa*: . . .

112 “Shikilia hicho ulicho nacho, Luther alikupokonya. Shikilia hicho, maana kinataka kufa. Utaninii. . . Watakutakasa urudi ndani yake tena. Shikilia hicho, kinataka kufa.”

113 Sasa:

. . . wala *sikuona matendo yako kuwa yametimilika bado mbele za Mungu*.

114 Hilo si linapendeza? Loo, jamani! Ninapenda hilo. “Si makamilifu.” Kwa nini? Walikuwa wamehesabiwa haki tu, Luther alihubiri kuhesabiwa haki; ilibidi utakaswe kisha ujazwe na Roho Mtakatifu. Ndipo hawakuwa mali yao wenyewe, walikamilishwa na Roho Mtakatifu ndani yao. Mkristo siye—siye aliye mkamilifu, ni Roho Mtakatifu aliye mkamilifu ndani yake. Mnaona? Hilo ndilo. . . Kama vile nimesema, “Si mlima mtakatifu, ni Mungu Mtakatifu juu ya mlima. Si kanisa takatifu, si watu watakatifu, bali ni Roho Mtakatifu Kanisani na ndani ya watu.” Hiyo ndiyo sehemu *Takatifu*, mnaona.

115 “Wala sikuona matendo yako kuwa yametimilika. Hujafikia ukamilifu.” Kwa sababu tunaona sasa kwamba walikuwa na kuhesabiwa haki papa *hapa*, kuhesabiwa haki. Nayo hii ilikuwa. . . La, samahani. Kuhesabiwa haki kuko papa *hapa* chini ya Luther; nao utakaso uko *hapa*; na huyu *hapa* Roho Mtakatifu. Mnaona? Sasa, hizo elementi tatu zilizofanya kazi katika nyakati hizo tatu za makanisa, hizo ndizo zinazohitajika kukamilisha kuzaliwa kukamilifu. Zilishika tu mimba kama seli zazi ndogo katika tumbo la uzazi la mama. Hiyo ni kweli, Roho Mtakatifu akija katika kuzaliwa.

116 Sasa nataka kuwaulizeni jambo fulani. Wakati kuzaliwa kwa kawaida kunapotukia, jambo la kwanza linalotukia ni lipi? Maji. La pili ni lipi? Damu. Hiyo ni kweli? Jambo linalofuata? Roho. Hiyo ni kweli.

117 Ni kitu gani kilichotoka katika mwili wa Yesu hapo alipokufa? Walimchoma ubavuni Mwake, ndipo maji na Damu ikatoka, “Na mikononi Mwako naiweka Roho Yangu.” Maji, Damu, Roho.

118 “Kwa hiyo tukiisha kuhesabiwa haki kwa imani,” Warumi 5:1, “tuna amani na Mungu kwa Bwana wetu Yesu Kristo,” kuhesabiwa haki. Kutakaswa, Waebrania 13:12 na 13, “Yesu aliteswa nje ya malango apate kuwatakasa watu kwa Damu Yake Mwenyewe.” Luka 24:49, “Lakini kaeni katika mji wa Yerusalemu mpaka mtakapovikwa uwezo utokao Juu. Akiisha kuwajilia Roho Mtakatifu, *basi* mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, Yuda, Samaria. . .”

119 Si wakati unapokuwa askofu, si wakati unapokuwa shemasi, si wakati unapokuwa mchungaji, si wakati unapokuwa papa,

“Lakini akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu, basi mtashuhudia.” Unaweza tu kushuhudia kanisa lako na kanuni yako ya imani, kama . . . kama wewe ni shemasi tu, ama kama wewe ni mchungaji tu, ama kama wewe ni papa tu, ama kama wewe . . . Unashuhudia kanuni ya imani! Lakini Roho Mtakatifu atakapokujilia, basi utashuhudia habari Zake! Na kazi alizofanya, utazifanya pia, kwa sababu Uzima Wake uko ndani yako. Loo, loo! Jamani, jamani! Namna hiyo. Naam, bwana. Loo, ninalipata zaidi . . . zaidi hapa juu, ninaamini, kuliko mnavyolipata huko nje. Ninajisikia tu vizuri Nalo.

120 “Mambo yanayotaka kufa, uyaimarishe.” Sasa yeye anasema hapa, sasa kwenye kifungu cha 3:

Basi kumbuka jinsi ulivyopokea, na jinsi ulivyosikia, . . . (Ninapenda hilo) . . . yashike hayo na kutubu. Walakini usipokesha, nitakuja kwako kama mwizi, wala hutajua saa nitakayokuja kwako ambayo . . . nitakuja kwako.

121 “Shika sana kuhesabiwa haki kwako, kushikilie.” Usiwaruhusu hao watu wakunyang’anye huko. “Hayo pia uliyopokea, ulisikia.” Walisoma Biblia ile ile tunayosoma, mnaona. Lakini hawakuichukua tu yote, kwa kuwa haikufunuliwa kwao. Haikuwa ni kwa ajili ya wakati wao. Hiyo ndiyo sababu watatokea kwenye ufufuo. Walitembea katika ile Nuru waliyokuwa nayo ya kutembelea, kwa hiyo watafufuliwa.

122 Sasa, nimewasikia Wapentekoste wengi wanaohubiri ubatizo, wakisema, “Hao Walutheri, na kadhalika, hawatafufuliwa.” Loo, naam. Mnajua ile hadithi ndogo kuhusu Dk. Hegre kule juu. Wakati nilipomwambia . . . Yeye alisema, “Sisi tuna nini?” Nikasema . . . Mwajua, waliinua seminari ile kuu ya Kilutheri huko, Bethany, huko Minneapolis. Basi akasema, “Vema, sisi Walutheri tuna nini?”

Nikasema, “Vema, nitakwambia. Ninaamini mnaye Kristo.”

Naye akasema, “Vema, tunataka—tunamtaka Roho Mtakatifu.” Akasema, “Je, unafikiri tunaye?”

Nikasema, “Kwa uwezekano.” Kisha nikasema, “Mnaamini mkielekea Kwake.”

Akasema, “Vema, una maana gani?”

123 Sasa, wana maelfu ya ekari pale ambazo wanafunzi wao . . . endapo hawawezi—hawawezi kujilipia masomo, waliwaruhusu kufanya kazi na kulima mahindi. Nikasema, “Vema . . .” Kuna—kuna meza kubwa tu. Walinipa moja ya hiki chakula maalumu cha jioni kule chini kwenye seminari hiyo kubwa. Na sasa, hao ni watu wazuri; Dk. Hegre ameketi *hapa*, na Ndugu Jack Moore *hapa*; maana nilimweka karibu ambapo kama akianza kuzungunza maneno makubwa nisiyoyajua, ningemgusa Jack

kwa mguu wangu nione kile alichosema, mnaona. Kwa hiyo basi, nikasema . . .

124 Aliketi karibu nami, ndipo akasema, “Vema, kile tunachotaka kufanya ni kutafuta kujua kitu fulani hapa.” Kasema, “Tuna njaa ya Mungu.” Kisha kasema, “Tulisoma kitabu juu ya Pentekoste, *Zile Karama*.” Tena kasema, “Tukaenda . . . baadhi yetu ndugu tuliruka kwa ndege hadi California, tukakutana na huyo mtu aliyekiandika kitabu hicho.” (Nami ninamjua.) Akasema, “‘Tungetaka kuona baadhi ya karama hizo zikitumika.’ Akasema, ‘Sina yoyote ya hizo,’ kasema, ‘niliandika tu kuzihusu.’” Kwa hiyo akasema . . . Kisha kasema, “Ndipo tulipokuja kule na kuona haya, tuna njaa. Tunamtaka Mungu.”

125 Ndipo nikasema, “Vema, siku moja alitokea mtu.” Mwajua, katika shamba lake mwenyewe pale, mnaona. “Mtu mmoja alitoka akaenda akalima shamba kubwa mno. Na akang’oa mizizi yote kwake, na kila kitu, kisha akapanda mahindi. Kila asubuhi alienda mlangoni na kuangalia aone kama alikuwa na mahindi yoyote. Muda si muda mwajua, asubuhi moja, majani mawili madogo yalikuwa yakitokeza.” (Mtu yeyote aliyewahi kulima mahindi . . . Yuko wapi George Wright na hao wengine, Roy Slaughter na hao wengine? Mwajua, hayo majani mawili madogo yanayochomoza.) “‘Loo,’ akasema, ‘Mungu asifiwe kwa ajili ya shamba langu la mahindi.’”

Nikasema, “Hivi alikuwa na shamba la mahindi?”

Akasema, “Vema, kwa njia moja.”

126 Nikasema, “Kwa uwezekano, ndiyo.” Nikasema, “Hiyo ilikuwa ni ninyi Walutheri katika yale matengenezo ya kwanza, mkizaa lile jani dogo la kwanza, mnaona.” “Vema,” nikasema, “muda si muda mahindi hayo yakakua.” Sikumwambia juu ya “mabaki,” mnaona, niliacha tu aendelee na mahindi, yalivyokua.

127 Kwa hiyo nikasema, “Hayo mahindi yakakua, na baada ya muda kidogo yakapata kishada. Ndipo hicho kishada kikaliangalia hilo tawi na kusema, ‘Ha-ha-ha-ha-ha, wewe huna chochote, maskini enyi Walutheri baridi.’ Mnaona? Kasema, ‘Mimi ni . . . Mimi—mimi ni mzalishaji, ule wakati mkuu wa kimishenari.’ Upepo ukavuma, ndipo maskini vishada vikaanguka namna hiyo na kuanguka chini; huyo ni Wesley, utakaso.” Mnaona? Huo ulikuwa ndio wakati mkuu sana wa umishenari tuliowahi kuwa nao, umekuwa ni kanisa la Kiwesley, kwenye wakati wa Wesley, hata unashinda wakati huu. Wakati wa Kanisa la Kiwesley, ulikuwa ni wakati wa umishenari, nao ulieneza. Ulifanya nini, u—ulilienneza.

128 Mnaona, hata maumbile yanashuhudia hizi tatu, papo hapo. Maumbile yenyewe, Mungu hapo mwanzo alilifanya kusudi liwe

hivyo. Haikubidi hata kuwa na Biblia, unaweza kuyaangalia maumbile na kuona mahali ulipo. Unaona?

¹²⁹ Halafu basi . . . Na hapo baada ya kitambo kidogo ikaanguka kule. Basi ni kitu gani kilichotokea? Likatokea shuke la mahindi, lilikuwa na punje juu yake; hilo lilikuwa ni kundi la Kipentekoste. Sasa, hilo kundi la Kipentekoste lilikuwa ni kundi la aina ile ile hapa *chini*. Kutoka *hapa* alikuwa na majani mawili ya mahindi, Luther; *hapa* alikuwa na kishada, Wesley; na *hapa* chini alikuwa na punje ya mahindi (Kitu gani?) jinsi hasa ilivyokuwa *hapa* nyuma. Kitu kile kile!

¹³⁰ Vema sasa, hiki kilikuwa ni kitu gani hapa? Mnasema, “Vema, sasa,” Mpentekoste alisema, “sina haja nawe Mmethodisti wala ninyi Walutheri.” Lakini, hata hivyo, uhai ule ule uliokuwa kwenye yale majani mawili madogo ulisaidia kufanya kile kishada. Na uhai uliokuwa katika kile kishada uliyafanya hayo mahindi. Kwa hiyo, mnaona, wote ni mpango wa Mungu. Walikuwa na Roho Mtakatifu, kwa uwezekano; vivyo hivyo na Wesley, chini ya utakaso; lakini siku hizi lilirejesha kunena kwa lugha, na kurudishwa kwa ule mwanzo *huku* nyuma. Roho Mtakatifu yule yule, mnaona, wale wa kweli. Amina. Naam.

¹³¹ Vema, “Shikilia sana yale ambayo umesikia, yasije yakafa.” Sasa kifungu cha 4, ninaamini ndicho:

Lakini unayo majina machache katika Sardi, watu wasioyatia mavazi yao uchafu; nao watakwenda pamoja nami hali wamevaa mavazi meupe: kwa kuwa wamestahili.

¹³² “Sasa, usiunde dhehebu kutoka Kwake, hatutaki kufanya hilo.” La, nina ninii . . . Ni—nimesoma kifungu kingine, sivyo? Ama sikusoma? Naam, naam, hiyo ni kweli. Naam. Vema. Naam, “Katika Sardi, hawajayachafua mavazi yao.” Kulikuwako na wachache wao ambao wangali wasingesujudia kitu hicho, nao wakajitakasa na kujisafisha; wale wa kale kutoka huko nyuma kabisa Pentekoste, waliojazwa na Roho. Wengi wao wakati huo, hapo wakati wa Luther ulipoanza kuunda dhehebu; wakafanya nini? Walianza kurudi moja kwa moja nyuma kama Biblia ilivyosema, “Wakitenda kama mama yao.” Wakashuka chini moja kwa moja, wakaunda dhehebu. Lakini wachache wao wakasimama moja kwa moja kwamba wasingefanya hivyo, wakaanza moja kwa moja kumtetea Mungu. Kasema, wakasema—kasema, “Vema, sawa, una majina machache, nao wanastahili kutembea mbele Zangu, wamevikwa mavazi meupe. Usiunde dhehehebu. Usilichukue fundisho la Wanikolai, sasa. Usiande kuunda dhehebu lako tena, bali kaa huru katika Mungu. Hebu Roho Mtakatifu awaongoze mnapoendelea. Kunao wachache wao waliosalia bado.”

¹³³ Sasa kifungu cha 5, ninaamini:

Aliye na sikio, na asi- . . .

134 Hebu tuone. La.

Yeye ashindaye, huyo atavikwa vazi jeupe; wala sitalifuta . . . jina lake katika kitabu cha uzima, bali nitakiri jina lake mbele za Baba, na mbele ya malaika.

135 Sasa, “majina machache.” Masalia wachache sana, wadogo, walisalia ambao hawakulichukua . . . kuchukua . . . hawakuchuliwa na mafundisho ya Katoliki. Vema.

136 Sasa tunakuja kuzungumza juu ya yale matengenezo. Ningetaka kuninii . . . Niliacha msingi wa Luther ili kwamba niweze kuuweka hapa. Sasa kifungu kifuatacho kilisema:

Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa.

137 Mungu, akijaribu kuwaonya hapa wakae nje ya Unikolai huu, “Kaeni mbali na hapo! Yawekeni mavazi yenu pasipo kutiwa madoo na mambo yoyote ya ulimwengu!” Kaeni tu huru ndani Yake, Naye angewaongoza na kuwaelekeza. Sasa, huo ndio mwanzo wa kwanza.

138 Sasa, kwa *matengenezo* ninamaanisha “wale walionusurika,” wale waliokuwa wamenusurika hata katika kanisa la Sardi. Mnaelewa yale ninayomaanisha? Wale ambao walikuwa wangali wamekitoroka kitu hicho kiovu sana. Sasa hiyo . . . Sasa, tutalichukua tena kesho usiku na kulishusha moja kwa moja hapa chini katika . . . katika wakati wa Kipentekoste, na kuwaonyesha huo ndio hasa. Sasa, kuna baadhi ya mambo haya, tunayozungumza habari zake hapa: kwamba “Wao waliutorokaje?” Sasa, tutalichukua hilo, chini kwenye wakati unaofuata. Mnaona, hatuna budi kulichukua kulifanya liendane pamoja. Usipofanya hivyo, basi u—u—u—unakosa kuwapa wa—watu . . . kulishindilia kwenye huo wakati ujao, unaona. Inakupasa kuwaacha walipate tu kama vile Biblia inavyoutoa hapa, mnaona. Vema.

139 Sasa, walionusurika ndio anaozungumza habari zao. Hao ni hawa papa *hapa*, kundi hili dogo sana hapa linaloishi kwa kuhesabiwa haki. Sasa angalieni! Walitoka, wakaiona Nuru, Luther akageuka moja kwa moja . . . Baada ya kifo cha Luther, si Luther; Luther kamwe hakuunda dhehebu; ilikuwa ni lile kundi nyuma yake. Wesley hakuunda dhehebu lolote; ilikuwa ni lile kundi lililomfuata. Wale waanzilishi wa kale wa Pentekoste kamwe hawakuunda dhehebu; ilikuwa ni lile kundi lililowafuata. Hao ndio wanaofanya hilo, mnaona, ni ile zamu ya pili inayofanya hilo. Malaika halisi wa Nuru kamwe hataunda dhehebu! Nanyi mtaona kwenye huu—kwenye wakati huu wa Kipentekoste ni kitu gani kinachotokea mwishoni mwa dhehebu hilo, pia; mnaona, wakati Roho Mtakatifu atakapotufunulia.

140 Sasa, Yeye alisema, “Unayo Nuru kidogo iliyosalia, ndogo tu, iko tayari kuzima; inafifia, ni kuhesabiwa haki tu, wanaweza kukuyumbisha kwa njia yoyote. Huna Uzima wowote bado, kwa sababu ulilichukua jina baya. Lakini wewe ni—wewe ni. . . angalau umenyakuliwa ukatolewa nje. Unaona, wewe ni. . . ume—umelitoroka kanisa la Kirumi. Umeyatoroka hayo mafundisho yote ya sharti, na angalau umetoka nje umbali huo.” Sasa, unaisoma Biblia ile ile. Sasa, bali Biblia ile ile inayofundisha Roho Mtakatifu. . . Yeye hakuwalaumu kwa kile walichokuwa nacho. Kasema, “Sasa hiyo ni. . . shikilieni hilo mpaka nitakapokuja. Mnaona, endeleeni tu kushikilia.”

141 Sasa, wakati huo wa kanisa ulianza yapata mwaka wa 1520, wakati kanisa Katoliki la Kirumi, la ulimwenguni kote lilipokuwa na mamlaka kamili. Hayo yalidumu mpaka tarehe thelathini na moja Oktoba (Kama mnayaandika.) tarehe thelathini na moja Oktoba, mwaka wa 1570 A.D., wakati Martin Luther alipozibandika tasnifu zake tisini na tano kwenye mlango wa kanisa huko Wittenberg, Ujerumani, na tangu wakati huo yale Matengenezo yakapamba moto. Mlipata tarehe hizo? Hebu nizitoe tena mpate kuwa na hakika. Tarehe thelathini na moja Oktoba, mwaka wa 1570 A.D., wakati Martin Luther alipozibandika tasnifu zake tisini na tano kwenye mlango wa kanisa huko Wittenberg, W-i-t-t-e-n-b-u-r-g, Wittenberg, Ujerumani. Tangu tarehe hiyo yale matengenezo yalianza, moto ukaanza kuruka. Aliliasi kanisa hilo la Katoliki amesimama pale, huo ukiwa mkononi mwake namna hiyo, akasema, “Ati huu ni Mwili mtakatifu wa Kristo? Ni mkate mwembamba na divai kidogo!” Na “puh!” akautupa sakafuni. Hiyo ni kweli.

142 Yeye alilipinga kanisa Katoliki, na ninii. . . lililoanza. . . ule mpokonyo mdogo uliotokea wakati huo. Vema, ninii. . . ulikuwa ukiendelea. Bali ulikuwa zaidi sana ni vi—vita vya nguvu za kisiasa kuliko ulivyokuwa kwa ajili ya Kanisa la kweli, kwa ajili ya kanuni za Kikristo. Walishindania tu haki za kisiasa kutoka kwenye kanisa na kuanzisha kanisa lingine. Hawakutengeneza, kutoka kwenye kanisa Katoliki kumrejsha Roho Mtakatifu na nguvu kanisani, kwa sababu walimkataa. Umhu? Ulikuwa ni mkutano wa kisiasa. Hapo ndipo ungetoshea hasa, “Una jina kuwa u hai, nawe umekufa.” Kwa maneno mengine, yeye alilitoa tu dhehebu la Kiprotetanti, hivyo tu. Alimtoa binti kutoka kwa kanisa. Kutoka kwenye. . . Alimtoa kahaba kutoka kwa kahaba mkuu. Hilo ndilo lilitukia hasa. Alimtoa Athalia kutoka kwa Yezebeli.

143 Sasa, mtu yeyote anayesoma yale Matengenezo anajua ndivyo ilivyo, kwa sababu yeye kwa urahisi. . . Baadhi ya kumbukumbu na utaratibu wa kale ambao. . . na sherehe, yeye—yeye kwa urahisi aliziangamiza, lakini kuhusu kumrejsha Roho Mtakatifu kanisani kama alivyokuwa *hapa* nyuma, yeye hakufanya hivyo. La, bwana. Vilikuwa zaidi sana ni vita vya

kisiasa kuliko vilivyokuwa vya kiroho. Ilikuwa ni siasa badala ya Roho Mtakatifu. Yeye alikuwa bado hajaingia Kanisani. Loo, ndugu, Yeye hakuwa amerudi; Yeye anarudia *hapa*, sio *kule* juu.

¹⁴⁴ Sasa, ilikuwa ni mkutano mkuu wa kisiasa, bali haikuwa ni kwa ajili ya Maandiko Matakatifu na—na Roho Mtakatifu. Ilikuwa ni mkutano wa kisiasa ambapo kweli aliondolea mbali baadhi ya kumbukumbu za sanamu ya msalabani, na “*Salaamu Maria*,” na yote hayo. Lakini angali alileta katekismo. Angali alitoa hii. . . Mnaitaje? Ibada za kuwekwa wakfu ama chochote kile kule chini walipofikia kwenye asubuhi ya Pasaka naye mchungaji anawatakia “Krismasi Njema,” mwajua. “Siwaoni tena mpaka wakati wa Krismasi,” alisema, mwajua. Hilo. . . loo, ibada ya kipa—kipaimara, ndiyo ninayojaribu kusema. Kuwapeleka chini na kuwapa kipaimara, kuwapa ushirika wa kwanza na kuwapa kipaimara. Hakuna kitu kama kipaimara. Kipaimara cha pekee kilichotajwa katika Biblia, wakati katika—katika Biblia, ni wakati Mungu alipolithibitisha Neno Lake kwa ishara na maajabu yaliyofuata. Huko ndiko kuthibitisha, sio thibitisho la kuwa mfuasi wa kanisa la Kilutheri, bali Mungu akilithibitisha Neno Lake ndani yako. “Naye Bwana alikuwa. . . alitenda kazi pamoja nao,” Marko 16, “akithibitisha Neno kwa ishara iliyofuata.” Huko ndiko kuthibitishwa kwa Kanisa la kipentekoste. Huko ni kuthibi-. . . Mungu hujithibitisha Mwenyewe hai, kama Mungu afanyaye miujiza Kanisani, kunena kwa lugha, kufasiri lugha, na kufanya mambo yale yale waliyofanya hapo mwanzo.

¹⁴⁵ Ninawachosha? [Kusanyiko linajibu, “La.”—Mh.] Vema. Sasa, angalieni, hawakuurejesha uamsho wa Roho Mtakatifu; walirudisha wakati mpya wa kanisa. Waliwarudisha waliopokonywa; waliotoroka kutoka kwenye ukasisi wa Kirumi, kufanyiza ukasisi wa Kiprotestanti. Hilo ndilo jambo tu walilofanya. Wakaruka moja kwa moja kutoka kwenye kikaango wakaingia motoni, mnaona. Ni—ni kweli. Kabisa.

¹⁴⁶ Yezebeli alimzaa tu binti. Na sasa msifikiri ninasema tu hili ku—kujifanya mwerevu, ninasema hili kwa sababu Biblia ilisema hivyo! Biblia, katika Ufunuo 17, ilisema, “Yeye alikuwa ni mama wa makahaba.” Yesu alisema hapa, “Kama tu vile Yezebeli alivyokuwa, ndivyo atakavyokuwa.” Naye aliwazaa binti ambao waliipotosha n—nchi ambayo ilikuwa haijapotoshwa. Sasa, hivyo ndivyo hasa Uprotestanti ulivyomfanyia Roho halisi wa Mungu, ulipotosha kitu hicho na kukirudisha moja kwa moja katika dhehebu lingine. Ambalo, Mungu akipenda, Jumapili asubuhi, ninataka kuwaonyesha kwamba—kwamba—kwamba walifanya sanamu ya mnyama, naye mnyama huyo alikuwa ni Rumi. Nao wakafanya sanamu kama *hiyo*. Ilikuwa ni kitu gani? Dhehebu! Loo, natumaini hilo linazama ndani ya mioyo ya watu.

147 Nanyi mnashangaa ni kwa nini nimelipinga dhehebu sana maishani mwangu mwote; sikujua mimi mwenyewe. Lakini ilikuwa ni kitu *Fulani* ndani yangu kikipaza sauti; ninsingeweza kukizuia. Nilishangaa, daima nilishangaa, ni kwa nini sikuzote niliwakemea wanawake hivyo? Mnaona? Maisha yangu yote. Sio ha- . . . Ninamaanisha . . . simaanishi wanawake halisi; ninamaanisha hawa *wanaodhaniwa kuwa*, mwajua, walioharibikiwa na maadili na kadhalika. Mwajua. Hao ndio mimi. . . kitu *Fulani* ndani yangu.

148 Nilipokuwa maskini mvulana mdogo, kijitoto, huko juu, ningewaona hao wanawake wakipanda kuja njiani, na nani wao. . . nilijua waume zao walikuwa huko nje wakifanya kazi, hao huko juu pamoja na jamaa fulani, wamelewa; kando ya barabara, nao wangewatembeza huku na huku barabarani, kuwatoa ulevi vya kutosha kwenda nyumbani, wakawapikie waume zao chakula cha jioni. Nilisema hawastahili risasi safi kuwapitia. Hiyo ni kweli. Nilisema walikuwa duni kuliko wanyama, hao ambao wangepanya kitu kama hicho. Nami. . . Nilipokuwa na umri wa miaka kumi na saba, kumi na minane, ningemwona m—msichana akishuka kuja barabarani, ningevuka upande ule mwingine, nikasema, “Huyo nyoka mwenye sumu anayenuka.” Mnaona? Nami ningalikuwa mchukiaji halisi, bali nilipompokea Mungu moyoni mwangu, Mungu aliniruhusu kujua ya kwamba Yeye yuna vito huko nje, Yuna kina mama halisi. Wote hawatajitia najisi namna hiyo; Mungu ashukuriwe kwa ajili ya hilo.

149 Nilipokuwa huko Afrika, nilipokuwa huko Uswisi, na nilipokuwa huko Rumi, ninaulizwa swali hili sana, “Ati, aisee, Ndugu Branham, hivi nyinyi nyote hamna mwanamke yeyote mwadilifu hata kidogo Marekani? Kila wimbo unaokuja huku, kuna jambo fulani chafu kuwahusu wanawake wenu.”

150 Nikasema, “Hao ni Wamarekani. Ila tunao Ufalme mwingine ulioko kule, huo ni Ufalme wa Mungu; hao ni mama wenye heshima kwelikweli.” Hakika!

151 Biblia ilisema, katika—katika manabii, ilisema. . . Ninaamini ilikuwa ni yapata mlango wa 5 wa Isaya, sina hakika, ingekuwa katika mlango wa 5 ama wa 6 pale; ikizungumza juu ya, “Heri yule binti wa Sayuni, atakayeyatoroka mambo hayo yote siku hiyo.” Jinsi angeshuka mtaani; angezikunja soksi zake ndefu; angetembea akiliza njuga; akijinyonganyonga namna hiyo, na mambo ambayo angefanya. Jinsi hasa wanavyofanya sasa, kikamilifu hasa. Wanavaa nguo kama mwanamume, ambalo ni chukizo kwa Mungu.

152 Niliona shirika la kidini, muda mfupi uliopita, likienda kuwa na. . . namna fulani ya kubarizi wanakokuwa nako kila usiku, nao wanawake hawa wote wakitoka wamevaa hizi kaptura mkur- . . . Ama—ama mna—ama mnaviitaje vitu hivyo?

Si kaptura, bali kitu hicho kingine. Naam, ni visukuma pedali. Ama vitu hivyo pale. Vyote kwenye. . . Wanahitaji pedali isukumwe, vema; ndugu, huo ni ubao wa yapata upana *huo*. Hiyo ni kweli. Kichwa hutoka kwenye. . . *Mtembea kwa miguu*, hiyo ni “kwa mguu wako,” na hilo ndilo wanalohitaji hasa. Hiyo ni kweli.

153 Lakini, loo, mnasema, “Vema, sasa, ninafikiri hiyo ni ya heshima zaidi kwa mwanamke kuvaa kuliko sketi.”

154 Mungu alisema, “Ni chukizo mbele Zake kwa mwanamke kuvaa vazi. . .” Na wakati mwanamke anapozikata nywele zake kama mwanamume. . . Mungu anamtaka mwanamke kuonekana kama mwanamke, avae kama mwanamke, atende kama mwanamke.

155 Wala hamtaki mwanamume kuwa na masharafa makubwa mno yakining’inia chini namna *hii*, halafu, kama bata aliyeketi nyuma ya kichwa chake namna hiyo. Yeye anamtaka aonekane kama mwanamume. Naam, bwana. Jamani, wanavaa kike sana hata ni vigumu kwao kujua wao ni wa jinsia gani. Ni—ni huzuni, hawa wahuni na kadhalika tulio nao siku hizi. Si ajabu tunaishi katika wakati wa mwisho, hakuna kitu kilichosalia katika ulimwengu huu ila Mungu kuimwaga ghadhabu Yake juu yake na kuuteketeza. Hivyo tu. Mungu mwenye haki na Mtakatifu asingeweza kufanya lingine lolote.

156 Wameidharau Damu ya Yesu Kristo! Wamejishindilia mafundisho ya sharti! Wameingia katika dhehebu! Na maskini. . . maskini baba mtakatifu fulani pamoja na ninii yake. . . maskini kapera mwenye ukosi uliopinduliwa, anakuja na kuwaambia, “Watoto wangu waliobarikiwa.” Hilo halina maana zaidi ya nguruwe kulisema.

157 Ninawaambia, kile tunachohitaji usiku wa leo ni kuirudia Biblia na Roho Mtakatifu, ndugu, na nguvu za Kristo aliyefufuka zije Kanisani zikifanya ishara na maajabu na miujiza. Amina! Hiyo ndiyo Injili. Naam.

158 Ulileta. . . kwa hiyo. . . Naam, hiyo ni kweli, ulileta. U—u—uamsho ulifanya mambo mazuri sana pale, huo uamsho. Bali haukumleta Roho Mtakatifu. Hawakumleta huyo mpaka kufikia kwenye wakati huu wa Laodikia, huko chini katika wakati wa Kipentekoste. Lakini kweli ulifanya jambo moja. Uamsho huu ulifanya mambo fulani ambayo Yeye alisema, “Usiyaache yafe sasa, yaimarishe na uendele kuyaongeza.” Mnaona?

159 Ulileta Biblia ya bure kwa watu tena. Wakati wa Kilutheri ulileta Biblia ya bure. Waliunda mtambo wao na kuanza kuupa ulimwengu Biblia. Mungu awabariki Walutheri kwa sababu ya jambo hilo! Naam, bwana. Waliirudisha Biblia mikononi mwa walei tena; ilikuwa ni kasisi peke yake. Hata hawakuruhusiwa kuiangalia; kwa sababu ilikuwa ni yale aliyosema papa, naye

alikuwa ni mungu; kwa hiyo chochote alichosema, hicho kilitosha.

¹⁶⁰ Kwa hiyo sasa, uamsho wa Kilutheri, kile walichotaka, ni “kuimarisha.” Sasa unayo Biblia mkononi mwako, sasa isome! Iamini! Usiiweke kwenye rafu, useme, “Vema, tunayo Biblia.” Hilo halitakufaidi kitu huko juu. Kuna Walutheri wengi sana katika Pentekoste siku hizi, wameiweka Biblia huku na kuchukua kile mtu mwingine anachosema kuihusu Hiyo. Ndugu, lisome Neno! “Yatafuteni Maandiko, kwa kuwa hayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi,” alisema Yesu. “Ndani yake mnadhani mna Uzima wa Milele.” Hilo ndilo jambo la kufanya: lisome Neno!

¹⁶¹ Sasa, Yeye alisema tu, “Lishikilieni Hilo, ninii...msi—msiache hilo liponyoke.” Na jambo lingine alilowataka washikilie, walikuwa na nguvu kidogo iliyosalia ndani yao, ilikuwa...Ule uamsho wa Kilutheri, jambo la pili ulilofanya, ulileta fundisho la kuhesabiwa haki kwenye nuru. Katoliki haichukui kuhesabiwa haki; ni kanisa Katoliki.

¹⁶² Ni kama tu yule kasisi, iliwabidi kumwondosha hewani hapa siku moja. Yeye alisema, “Hamna wokovu mahali pengine popote ila katika kanisa Katoliki.” Wokovu uko ndani ya Kristo; si katika kanisa Katoliki, sio katika kanisa la Kiprotestanti. Uko ndani ya Kristo, wokovu. Lakini Katoliki inaamini... Hawajali yale Biblia isemayo; ni yale kanisa lisemayo. Mnaona? Huwezi kushauriana nao, kwa sababu hakuna njia—hakuna njia ya kuzungumza nao. Hawajali. Wana ninii...Watazungumza nawe juu ya katekismo yao, chochote kama hicho; bali ukiiendea Biblia, wao—wao wanaikataa tu Hiyo, “Ni yale kanisa lisemayo.”

¹⁶³ Lakini Yesu alisema, katika jambo lili hili, Yesu Mwenyewe alisema, “Kama mtu yeyote ataondoa lolote au kuongeza lolote Kwake, Yeye ataiondoa sehemu yake katika Kitabu cha Uzima.” Yesu alisema, “Neno la kila mwanadamu na liwe ni uongo, na Langu liwe Kweli. Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe.” Hiyo ni kweli? Loo, Hilo hapo, ndugu.

¹⁶⁴ Mimi ni mwaminio wa Neno la Mungu! Hiyo ni kweli. Wala sio tu hilo Neno ambalo Mungu analinena *pale*, kisha nilimwomba Baba wa Mbinguni kunipa Roho Mtakatifu *kulithibitisha* Neno hilo, kumfanya Kristo aishi ndani yangu. Ndipo nijue ninao Uzima wa Milele, sio kwa sababu ninaustahili, ni kwa sababu neema Yake imenipa Huo. Huo ndio mwamba. “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu,” Yeye alisema.

¹⁶⁵ Vema, kuhesabiwa haki. Vema. Jambo ni kwamba, baada ya kuleta jambo ambalo haiwapasi kuliacha life, hilo lilikuwa, walikuwa wanayo Biblia mkononi mwao tena. Walutheri walifanya hilo. Na jambo lingine, walikuwa na fundisho la “kuhesabiwa haki kwa imani.” Hivyo ndivyo Luther

alivyofundisha, kila mtu anajua ya kwamba hilo lilikuwa ndilo fundisho lake. Kuhesabi-...Hivi hamwezi kuona jinsi hilo lilivyokuwa ni kamilifu? Ndipo akaja Wesley pamoja na utakaso, kisha hii hapa Pentekoste inakuja pamoja na ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kikamilifu tu. Sasa mimi. . .

¹⁶⁶ “Unayo mambo machache, yashikilie sasa, wala—wala usiyaache yafe. Kama hutayashikilia hayo, nitakuja upesi kama mwivi nawe utarudi moja kwa moja katika dhehebu tena.” Na hivyo ndivyo walivyofanya, vivyo hivyo hasa, wakarudi moja kwa moja mle. “Umerudi moja kwa moja kwenye Unikolai tena, maana utarudi moja kwa moja kwenye madhehebu. Shikilia! Endelea kuisoma Biblia hiyo, na udumishe kuhesabiwa haki, na uendeleo kukaza mwendo.” Lakini kuna masalia wachache waliotoka mle. Masalia wachache.

¹⁶⁷ Baada ya, wa kwanza kuja, Luther; na ndipo akaja Zwingli; na kuendelea, Calvin; na kuendelea, na kadhalika, hata kufikia kwa Wesley. Lakini kulikuwako na wachache waliosalia waliotoka kule waliofundisha utakaso. Na kutoka kwa utakaso wakaja masalia wachache walioingia katika Roho Mtakatifu. Mnaona, maskini masalia hao, kotekote kule, wakilidumisha Hilo—Hilo hai. Vema.

¹⁶⁸ Lakini, la tatu, walileta namna nyingi sana za mafundisho ya kipagani, wakaja nayo, kama vile madhehebu, ubatizo wa uongo. Sasa, walikuja wakinyunyizia na kadhalika namna hiyo, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Wakaleta katekismo. Hakika walikuwa. . .kweli wanalistahili lile jina. . .pamoja na. . .yale Yesu aliyosema hapa, “Una jina la kuwa hai, bali umekufa.” Hiyo ni kweli. Vema.

¹⁶⁹ La nne, ni kweli kwamba matengenezo yaliondolea mbali mengi ya kumbukumbu zao zilizopigwa msasa na—na taratibu za ibada za dini na kadhalika, bali yakashindwa kanisani pamoja na kule kurudishwa kwa kuleta marekebisho, yalishindwa kurudisha mafundisho ya Injili yote pamoja na ishara zikifuata. Kanisa la Kilutheri kamwe halikuwa nayo. Kamwe hawakuwa nayo; wala kamwe hawakuwa nayo katika wakati wa Wesley. Walikuwa nayo tu katika mwisho wa wakati huu wa Laodikia.

¹⁷⁰ Sasa, tunapongia katika hilo, tutarudi moja kwa moja katika Maandiko na kuwaonyesha jinsi hasa walivyoliahidi. Hawakuwa na ninii. . .hawakuurejesha uamsho wa Roho Mtakatifu.

¹⁷¹ Kweli waliziacha sanamu; na kuziacha sanamu, hiyo ni kweli. Waliziondoa sanamu kanisani: Mariamu, na Yusufu, na—na Petro, na Paulo, na hizo zote. Waliziacha sanamu, bali hawakumgeukia Kristo aliyefufuka. Luther aliwaondoa kwenye sanamu, lakini akawaingiza kwenye kitu kama siasa ama—ama

dhehebu ama shirika, kujifanyia dhehebu lingine tu (sanamu kama ile ya kwanza) na kujaribu kulipanua zaidi kwa dhehebu.

172 Na sasa wangali wanapiga vita. Methodisti ingali inataka kuninii... Wabaptisi wote wawe Methodisti. Na Walutheri wote wanataka Wabaptisti wote na Wamethodisti wawe Walutheri. Pentekoste inataka Wabaptisti wote, Mlutheri, na kila kitu kingine, wawe Wapentekoste. Mnaona, mnaendelea tu kuongezea kwenye dhehebu lenu. Lakini huo sio mpango wa Mungu kwanza. Mpango wa Mungu wa kurudishwa ulikuwa ni kurudisha kile kilichokuwapo hapo mwanzo.

173 Angalieni! Kukifufua hicho! Kama kitabu hiki kikianguka sakafuni, sasa kuchukua kitabu kingine kichukue mahali pake sio kurudishwa, ufufuo. Inakubidi ukiinue *kile kile* juu. Amina. Kwa hiyo ikiwa kanisa lilikufa kupitia katika Wakati wa Giza na likawa pagani kabisa *hapa* nyuma, basi kurudishwa, ninii... Hayo ni matengenezo, kutengeneza; bali *kutengenezwa*, na *kuzaliwa mara ya pili*, ni mambo mawili tofauti. Mnaona? Waliyarudisha matengenezo, kutengeneza, kuziondokea sanamu zao nyingi na kadhalika, bali kamwe hawakumrudisha Roho Mtakatifu kanisani. Loo, Jina la Bwana libarikiwe! Ndugu, dada, unaweza kuliona? Kamwe hawakumrudisha Roho Mtakatifu, kwa maana yule ambaye kweli anaita Nuru ya kweli ya Injili... Vaa kofia yako sasa. Yule ailetaye Nuru ya kweli ya Injili ni malaika wa kanisa *hapa* chini. Sasa, tutaliona hilo Jumapili.

174 Sasa, watakuwa na taa juu ya taa, na taa za Kikristo, bali kila mmoja wao atarudi moja kwa moja katika dhehebu hilo. Lakini kutakuwako na mmoja atakayesimama dhidi yake. Naam, bwana. Naye atawakutua waliosalia kutoka huko hakika tu kama ninavyosimama kwenye mimbara hii. Hiyo ni kweli. Naye atarudi moja kwa moja kwenye mwanzo. Nami nitayachukua Maandiko kutoka kwenye Agano la Kale na Agano Jipya na kuwathibitishia ya kwamba yeye atafanya hivyo, malaika wa kanisa la Laodikia, hiyo ni kweli, atarudi moja kwa moja kwenye la asili na kukifufua kitu hiki hapa tena. Nao huo ufufuo utakuja kwenye siku ya huu *hapa*. Hiyo ni kweli.

175 Lakini Luther alilikutua kanisa likatoka, walionusurika. Walionusurika *moja*, hatua moja, utaka... kuhesabiwa haki. Walionusurika, aliutoa mguu mmoja kutoka kwenye upagani. Hiyo ni kweli. Wakati huo mwingine, miguu miwili ikatolewa. Hivyo tu.

176 Ni kama tu... Mliona katika Biblia kuna—kuna maji yanayotoka nyuma ya lile Hekalu? Naye alisema aliona maji yakifikia magotini mwake; halafu tena, maji yakamfikia kiunoni mwake; ndipo wakati huo mwingine, yakapitia kichwani mwake. Lakini yalipopitia juu ya kichwa chake, ilibidi afikie mahali angaliweza kuogelea. Mnaona, ilimbidi kuogelea.

177 Kwa hiyo tunafikia mahali sasa ama ni kuogelea au kuzama. Hivyo tu. Yatakuzamisha na kukupeleka mbali kabisa, ama kukuingiza ndani, mojawapo. Kwa hiyo, ni kuogelea au kuzama! Haleluya! Loo, nina furaha sana kwa ajili ya Roho Mtakatifu! Nawe je?

Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
mimi ni mmoja wao.
Mimi ni mmoja wao. . . (Akina nani *wao*? Sio
hawa, wale, ama wale, ama wale.)
. . . nina furaha sana kwamba ninaweza
kusema mimi ni mmoja wao, Haleluya;
Mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
mimi ni mmoja wao.

Hilo si linasikika ni zuri? Sikilizeni:

Walikuwa wamekusanyika katika chumba cha
juu,
Wote wakiomba katika jina Lake,
Walibatizwa kwa Roho Mtakatifu,
Na nguvu za utumishi zikaja;
Sasa yale aliyowafanyia siku hiyo
Atakufanyia yayo hayo,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
mimi ni mmoja wao.

Loo, mmoja wao, mimi ni mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
mimi ni mmoja wao, Haleluya;
Mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
mimi ni mmoja wao.

178 Wanaenda kwenye seminari? La. Baadhi yao hata hawawezi kuandika jina lao wenyewe. Hiyo ni kweli. Petro asingeweza. Biblia ilisema yeye alikuwa asiye na elimu wala maarifa, yeye na Yohana. Lakini iliwabidi kuwasikiliza wao, maana walijua walikuwa pamoja na Yesu.

Ingawa watu hawa huenda wasijifunze kuwa
(Wenye elimu.),
Wala kujivunia umaarufu wa kilimwengu
("Loo, Mungu abarikiwe, nina *ninii* kadha
wa kadha."),
Wote wamepokea Pentekoste yao,
Wakabatizwa katika Jina la Yesu;
Nao wanatangaza sasa, mbali na kwa upana,
Nguvu Zake zingali ni zile zile,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
mimi ni mmoja wao.

Loo, mmoja wao, mmoja wao,
 Nina furaha sana kwamba naweza kusema
 mimi ni mmoja wao;
 Mmoja wao, mmoja wao,
 Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
 mimi ni mmoja wao.

179 Hivi huna furaha kwake? Furaha sana kuwa mmoja wao. Afadhali niwe mmoja wao kuliko chochote nijuacho. Loo, ni afadhali niwe mmoja wao kuliko kuwa Rais wa Marekani ama niwe mfalme wa ulimwengu. Ninge. . . Kama Bwana Yesu angeshuka hapa chini, aseme, “Nitakurejesha kwenye umri wa miaka ishirini na kukufanya kiongozi, mfalme wa ulimwengu wote, na kukupa miaka elfu kumi ya—ya maisha juu ya nchi, kudumu mwenye umri wa miaka ishirini; kamwe usiwe na siku uliyo mgonjwa, huzuni, na yote yatakuwa ni furaha na kadhalika, na mfalme wa ulimwengu mzima, kuishi miaka elfu kumi; ama ungetaka kuwa mmoja wao na kusumbuka maishani kama unavyofanya?”

180 Ningesema, “Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao!” Baada ya miaka elfu kumi, basi nini? Lakini Huu ni wa Milele. Ulikujaje, ndugu? Loo, Huo umepitia kwenye Damu. Hiyo ni kweli. Umetoka mbali, na umekuja kwa Mungu kufanyika mwili na kukaa miongoni mwetu:

Katika hori zamani za kale, ninajua ni kweli kabisa,
 Mtoto mchanga alizaliwa apate kuwaokoa watu kutoka dhambini mwao.
 Yohana alimwona ufukoni, Mwana-Kondoo wa milele,
 Loo, Kristo, aliyesulubiwa wa Kalvari.

Loo, nampenda yule Mtu wa kutoka Galilaya, kutoka Galilaya,
 Kwa kuwa amenifanyia mambo mengi sana.
 Amesamehe dhambi zangu zote, akamweka Roho Mtakatifu ndani;
 Loo, nampenda, nampenda yule Mtu wa kutoka Galilaya.

Yule mwanamke pale kisimani, Yeye alimwambia dhambi zake zote, (Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.)
 Na jinsi alivyokuwa na waume watano wakati huo.
 Alisamehewa kila dhambi, na amani kuu ikawekwa ndani;
 Akalia, “Njoni mmwone Mtu huyu wa kutoka Galilaya!”

Loo, nampenda yule Mtu wa kutoka Galilaya,
kutoka Galilaya,
Kwa kuwa amenifanyia mambo mengi sana.
Amesamehe dhambi zangu zote, akamweka
Roho Mtakatifu ndani;
Loo, nampenda, nampenda yule Mtu wa
kutoka Galilaya.

Mtoza ushuru alienda kuomba kule hekaluni
siku moja,
Akalia, “Ee Bwana, unirehemu!”
Alisamehewa kwa ajili ya kila dhambi, na
amani kuu ikaingia ndani;
Akasema, “Njoni mmwone Mtu huyu wa
kutoka Galilaya.”

Ninapenda hilo. Nanyi je?

Wiwete walifanywa kutembea, bubu
walifanywa kuzungumza,
Nguvu hizo zilinenwa kwa upendo baharini;
Na vipofu walifanywa kuona, ninajua
ingeweza tu kuwa ni
Rehema za yule Mtu wa kutoka Galilaya.

Uimbeni pamoja nami:

Loo, nampenda yule Mtu wa Galilaya, wa
Galilaya,
Kwa kuwa amenifanyia mambo mengi sana.
Amesamehe dhambi zangu zote, akamweka
Roho Mtakatifu ndani;
Loo, nampenda, nampenda yule Mtu wa
Galilaya.

¹⁸¹ Hivi hamuupendi? Loo, jamani! Hii Injili nzuri, ya Roho Mtakatifu, loo, jinsi ninavyoipenda. Ninapenda kwa moyo wangu wote. Nami nina furaha sana usiku wa leo ya kwamba nimehesabiwa pamoja nao, nasi tuko pamoja kama ndugu na dada. Wabaptisti, Wamethodisti, Pres-. . .Katoliki, Presbiteri, wowote wale, Mungu amettoa kutoka kwenye kila tabaka la maisha na ametuleta huku kwenye ushirika huu mkuu wa Roho Mtakatifu. Sio kuwa wafuasi wa dhehebu lolote, wafanyayo ni juu yao, bali sisi tuko katika Ufalme wa kisiri. Tumebatizwa katika mwili wa kisiri wa Yesu Kristo, kwa Roho Mtakatifu. Ni akina nani? Mmethodisti, Mbaptisti, Mpresbiteri, yeyote atakaye, na aje.

¹⁸² Yesu alisema, “Wote alionipa Baba watakuja Kwangu, wala hakuna mmoja wao atakayepotea, Nami nitawafufua tena katika siku ya mwisho.” Loo, jamani! Tulizoea kuimba wimbo wa kale hapa madhabahuni; sijui kama tunaweza kuuimba ama la, “Nafasi, nafasi, naam, nafasi ipo, ipo nafasi kwenye chemchemi kwa ajili yangu.” Mnazipenda hizo nyimbo za kale

namna hiyo? Mtu fulani atupe sauti, mtu fulani anayejua jinsi ya kuanzisha. Mpiga piano wetu yuko wapi? Yuko hapa? Ama Ndugu Teddy ama yeyote wao hapa? Hao? Loo, jamani, si-simwoni mahali popote.

Nafasi, nafasi, ndiyo, kuna nafasi,
Ipo nafasi kwenye chemchemi kwa ajili yako;
Nafasi, nafasi, ndiyo, kuna nafasi,
Ipo nafasi kwenye chemchemi kwa ajili yako.

183 Mnazipenda nyimbo hizo za kale? Tena ninaupenda huu pia:

Kule chini msalabani alipofia Mwokozi wangu,
Kule chini nililia nipate kusafishwa kutoka dhambini;

Loo, hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;
Utukufu kwa jina Lake!

Utukufu kwa jina Lake! Jina Lake la thamani!
Loo, utukufu kwa... (Hebu tuyafumbe tu macho yetu sasa na kuuimba.)

Loo, hapo damu ilipakwa moyoni mwangu;
Utukufu kwa jina Lake!

Nimeokolewa kutoka dhambini kiajabu,
Yesu anaka ndani vizuri sana,
Pale msalabani ambapo alinichukua;
Utukufu kwa jina Lake!

Utukufu kwa jina Lake! Hilo Jina la thamani!
Utukufu kwa jina Lake! Jina la thamani!
Hapo damu ilipakwa moyoni mwangu;
Utukufu kwa jina Lake!

184 Sasa wakati tukiimba kifungu hiki kingine, peaneni mikono na mtu aliye mbele yako, nyuma yako, kando yako.

Njoni, kwenye chemchemi hii iliyo tajiri na tamu;

Itupe maskini nafsi yako miguuni pa Mwokozi;
Loo, jitumbukize leo hii, na ufanywe mzima;
Utukufu kwa jina Lake!

Utukufu kwa jina Lake! Hilo jina la thamani!
Utukufu kwa jina Lake la thamani!
Hapo damu ilipakwa moyoni mwangu;
Utukufu kwa jina Lake!

Loo, naupenda huo. Nanyi je?

Utukufu kwa jina Lake! Jina la thamani!
Utukufu kwa jina Lake!
Hapo damu ilipakwa moyoni mwangu;
Utukufu kwa jina Lake!

185 Loo, jamani! Nina furaha sana kwa ajili ya jambo hilo. Nanyi je? Nina furaha sana kwamba ninaweza kuja kwenye

Chemchemi hii iliyo tajiri na tamu, nitupe maskini nafsi yangu miguuni pa Mwokozi.

¹⁸⁶ Ninakumbuka siku moja, nilipokuwa mvulana mdogo, yapata umri wa miaka kumi na minane, nikimkimbia Bwana. Nilienda Magharibi, nilitaka...Baba yangu alikuwa ni mwendesha farasi, nami nilitaka kwenda huko kuwafunza farasi. Kitu fulani tu kikiona njaa moyoni mwangu. Loo, nawaambia!

¹⁸⁷ Nilishuka nikaenda kwa mhubiri wa Kibaptisti, yeye akasema, “Simama na kusema tu, ‘Yesu ni Mwana wa Mungu,’ tutaliandika jina lako kwenye kitabu.” Hilo halikuniridhisha mimi.

¹⁸⁸ Kila mahali nilipoenda mtu fulani...Mwadventista wa Sabato, nilienda kumwona, mtu mzuri, Ndugu Barker, ndugu mpendwa, yeye akasema, “Billy, njoo ukaikubali sabato ya Bwana.” (Nimeikubali sasa.) Lakini yeye akasema, “Siku ya sabato.” Ndipo nikawazia, “Loo, jamani, hilo lingali halilitimizi.” Mnaona.

¹⁸⁹ Nikatoka nikaenda Magharibi, nami nikawazia... Nikaenda huko mbali sana kule nyuma usiku huo, tulikuwa tukiwakusanya. Na, mwajua, uliondoa matandiko pamoja na mkoba wako wa kambi, na kuutandika, kisha ukatumia matandiko yako kama foronya. Nami nilikuwa nimejilaza chini, chini ya hiyo misonobari usiku huo. Nami nilikuwa kwenye zamu ya mchana, na kwa hiyo wavulana wa usiku walikuwa huko nje wakiwaleta ng’ombe. Basi kulikuwako na maskini jamaa mmoja jina lake “Slim,” kutoka Texas, alikuwa na gi—gita pale naye alikuwa akipiga:

Utukufu kwa jina Lake!

¹⁹⁰ Jamaa mwingine pale alikuwa na kichanuo pamoja na kipande cha karatasi, akikipulizia. [Ndugu Branham anavumisha, *Utukufu kwa Jina Lake*—Mh.] Walikuwa wakiimba nyimbo zingine, vitumbuizo vya kaoboi, kisha wakaanza kuuimba huo *Huko Chini Msalabani*.

¹⁹¹ Jamani! Nikageuka, nikaiweka blanketi yangu juu ya kichwa changu namna *hii*. Nikaangalia huko nje nyuma, mwajua, na ilionekana kama hizo nyota zilikuwa zikining’inia moja kwa moja kule chini karibu na vichwa vya miti hiyo na milima hiyo. Maskini mnong’ono huo usio na mwisho wa misonobari hiyo, ningeweza kumsikia Yeye akipaza sauti, “Adamu, uko wapi?”

¹⁹² Yapata majuma matatu baada ya hapo, nilishuka mjini na hao wavulana wote wakalewa, wala mimi sikunywa. Ingenibidi kuwarudisha wote nyumbani, niwapakie kwenye gari, kwa njia yoyote. Nao wanatoka huko nje na kurushiana risasi kwenye vidole vya miguu mmoja kwa mwingine, na kadhalika, na ni hatari kuwa salama; kuchora mstari mnyofu kupitia pale,

na kuweka dau dola tano kila mmoja kwamba wangeweza kutembea juu yake, wala wasingeweza kutembea kwenye kinjia huko nje namna hiyo, mwajua. Na hivyo ndivyo ilivyokuwa mpaka wote walipotoa ulevi, baada ya kupata fedha zao.

¹⁹³ Nami nilikuwa huko chini na wote walikuwa wakinywa pombe, nikaenda kando na kuketi chini. Nikawazia, “Jamani, jamani!” Yapata miaka thelathini na mitano iliyopita, ama thelathini na mitano, nadhani, miaka thelathini na mitano iliyopita. Ndipo nikaketi chini pale, kando. Phoenix palikuwa ni mahali padogo wakati huo, tulitoka Wickenburg huko chini. Nilikuwa nimeketi kule chini, na kulikuwa na msichana mdogo wa Kihispaniola aliyepitia pale akijinyonganyonga; nami nimeketi pale pamoja na kofia hii kubwa nyuma ya kichwa changu; akapita hapo na kuangusha maskini lesi hii ndogo, mwajua. Nikasema, “Aisee, umeangusha lesi yako.” Halikunivutia.

¹⁹⁴ Nikasikia kelele kidogo chini ya mtaa pale, nami nikashuka kule. Basi palikuwapo na maskini mvulana aliyeongoka kutoka kwenye vibanda vya kurukia farasi huko nje, viduduiko vimeufunika uso wake, nayo machozi yakitiririka chini ya mashavu yake pale, akicheza gita, akiimba:

Utukufu kwa jina Lake!

¹⁹⁵ Loo, jamani! Machozi yakitiririka usoni mwake, akanyamaza na kusema, “Ndugu, hujui ni kitu gani mpaka umempokea huyu Kristo wa ajabu”:

Utukufu kwa jina Lake!

¹⁹⁶ Nami nikavuta hiyo kofia kubwa chini na kuondoka. Loo, jamani! Huwezi kujificha kutoka Kwake. Afadhali ujitokeze na kumkiri. Loo, Yeye ni wa ajabu! Naam, ndivyo alivyo.

Nimeokolewa kutoka dhambini kiajabu,
Yesu anakaa ndani kwa utamu, (*hukaa* ndani)
Pale msalabani ambapo alinichukua;
Utukufu kwa jina Lake!

Utukufu kwa jina Lake! Jina!
Utukufu kwa jina Lake!
Loo, hapo damu ilipakwa moyoni mwangu;
Utukufu kwa jina Lake!

Loo, njoo, kwenye chemchemi hii tajiri na
tamu;
Itupe tu maskini nafsi yako miguuni pa
Mwokozi;
Loo, jitumbukize leo hii, na ufanywe mzima;
Utukufu kwa . . .

Sasa na tuinamishe vichwa vyetu, tuiinue tu mikono yetu sasa:

Utukufu kwa jina Lake! (Utukufu, utukufu!)
 (Ee Mungu.) . . . Jina la thamani!
 Hapo damu ilipakwa moyoni mwangu;
 Utukufu kwa jina Lake!

197 Utukufu kwa Mungu! Na tusimame. Loo, hebu kidogo tu; ninii tu, ngojeni tu. . . [Dada fulani ananena kwa lugha nyingine. Ndugu mmoja anafasiri—Mh.] Naam, Bwana.

198 Sasa kama kungekuwako na wengine ambao wasingejua hiyo ilikuwa ni nini, hiyo ni Pentekoste, Roho Mtakatifu akizungumza. Yesu alisema, “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Watanena kwa lugha mpya; wataweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya.” Mambo haya yote anayonena habari zake, yatatimia.

199 Loo, nina furaha sana. Mnamwona Roho Mtakatifu akija, akilithibitisha Neno? Nuru, ichukueni, msi—msiitilie shaka. Ipokeeni tu Naye atawashughulikia kama mtoto na kuwaleta moja kwa moja huku juu. Hilo si ni zuri kwa Roho Mtakatifu kufanya hivyo? Roho Mtakatifu juu yetu.

200 Ninakumbuka wakati mmoja katika Biblia, hawakujua kitu hicho kilikuwa kikija kupitia wapi, adui alikuwa akija, ndipo Roho Mtakatifu akashuka juu ya mtu fulani namna hiyo, akawaambia mahali hasa pa kwenda. Nao wakaenda kule, ndipo Mungu akalivuruga hilo jeshi lingine na kuliangamiza. Hiyo ni kweli.

201 Loo, tungali tunaishi katika siku za Biblia! Sivyo? Amina. Daima, mradi tu Roho Mtakatifu yupo.

202 Loo, hebu tusimame tunapimba:

Peleka jina la Yesu. . . (Ukumbukeni ule
 Ujumbe.)
 Mtoto wa huzuni na wa majonzi;
 Litakupa furaha na faraja,
 Peleka uendako.

Jina la thamani, Jina la Thamani,
 Loo ni tamu jinsi gani!
 Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
 Jina la thamani, Hilo Jina la thamani!
 Ni tamu jinsi gani!
 Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

Peleka jina la Yesu,
 Kama ngao dhidi ya kila mtego;
 Majaribu yatakapokuzingira,
 Taja jina hilo takatifu katika maombi. (Mungu
 asifiwe!)

Jina la thamani,
 Loo ni tamu jinsi gani!
 Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
 Jina la thamani, Jina la thamani, Loo ni tamu
 jinsi gani!
 Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

Sikilizeni kufungu hicho:

Peleka jina la Yesu,
 Kama ngao dhidi ya kila mtego;
 Majaribu yanapokuzingira,
 Taja jina hilo takatifu katika maombi.

Loo, hebu tuuimbe tena:

Peleka jina la Yesu,
 Kama ngao dhidi ya kila mtego;
 Majaribu yatakapokuzingira,
 Taja jina hilo takatifu katika maombi.

Hebu tuinamishe vichwa vyetu sasa:

Jina la thamani, Jina la thamani, Loo ni tamu
 jinsi gani!
 Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
 Jina la thamani, Loo ni tamu jinsi gani! Tamu
 jinsi gani!
 Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.



WAKATI WA KANISA LA SARDI SWA60-1209
(The Sardisean Church Age)

MFULULIZO WA UFUNUO WA YESU KRISTO

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Ijumaa jioni, tarehe 9 Desemba, 1960, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org